# SIFA ZA KIUHALISIAJABU NA UMUHIMU WAKE KATIKA *UTENZI WA MWANA FATUMA.*

**NA**

**FLORENCE LUDIA VUTAGWA.**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUTOSHELESHA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**IDARA YA LUGHA NA ISIMU.**

**NOVEMBA, 2013.**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

______________________________ __________________________

Florence Ludia Vutagwa. Tarehe

NAMBARI YA USAJILI. C50/66305/2011

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Nairobi.

________________________________ _________________________

Prof. Kineene Wa Mutiso. Tarehe

(Msimamizi)

________________________________ _________________________

Dkt. Amiri Swaleh Tarehe

(Msimamizi)

## TABARUKU

Tasnifu hii nawatabarukia mume wangu mpendwa John Makokha Nyukuri na wanangu Joshua, Faith, Daniel na Peshe.

# SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na uwezo wa kuyaendeleza masomo yangu. Pasipo yeye safari hii singeliiweza. Shukurani zangu za dhati pia ni kwa wasimamizi wangu Prof. Kineene Wa Mutiso na Dkt. Amiri Swaleh kwa kunipa mwelekeo tangu mwanzo hadi tamati.

## YALIYOMO

UNGAMO....................................................................................................................... ii

SHUKRANI.................................................................................................................. iv

YALIYOMO.................................................................................................................. v

**SURA YA KWANZA** ............................................................................................ **1**

**1.0 UTANGULIZI**........................................................................................................ **1**

1.1 Tatizo la utafiti.......................................................................................................... 4

1.2 Malengo ya utafiti. .................................................................................................... 4

1.3 Sababu ya kuchagua mada ........................................................................................ 4

1.4 Nadharia tete. ............................................................................................................ 5

1.5 Upeo na mipaka. ....................................................................................................... 6

1.6 Msingi wa Nadharia .................................................................................................. 6

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Somo. ................................................................................. 10

1.8 Njia za utafiti........................................................................................................... 16

1.9 Hitimisho................................................................................................................. 17

**SURA YA PILI**........................................................................................................ **18**

**MUHTASARI WA *UTENZI WA MWANA FATUMA* NA MATUKIO YA KIAJABU.**..... **18**

2.0 Utangulizi................................................................................................................ 18

2.1. Mazoea ya Mtunzi................................................................................................... 19

2.2 Maombi, sifa za Allah na maajabu ya uumbaji........................................................ 20

2.3 Sifa za Mtume Muhammad...................................................................................... 21

2.4 Maudhui ya utenzi na vinne bora............................................................................. 22

2.5 Fatuma kama kielelezo bora cha wanawake wote ulimwenguni ............................. 24

2.6 Uhusiano kati ya Ali na Muhammad. ...................................................................... 26

2.7 Allah anaamuru matayarisho ya harusi. 26

2.8 Ufafanuzi juu ya harusi 27

2.9 Ndoa takatifu mbinguni na duniani 27

2.10 Safari ya kutoka Shamu kurudi Madina 28

2.11 Wasia wa Fatuma 29

2.12 Matukio ya kiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* 29

2.13 Uzuri wa Fatuma 30

2.14 Uhusiano wa Mtume Muhammad na Binti yake Fatuma 31

2.15 Posa ya Fatuma 32

2.16 Matayarisho ya ndoa ya Fatuma 33

2.17 Maisha ya Ali 37

2.18 Hitimisho 39

**SURA YA TATU** 43

**SIFA ZA KIUHALISIAJABU KATIKA *UTENZI WA MWANA FATUMA*.** 43

3.0 Utangulizi 43

3.1 Matukio yaliyo ya kiajabu ambayo ni ya kushangaza na ya kuogofya. 43

3.2 Kuvunjwa kwa mipaka ya mahali 46

3.3 Matukio yanayozungumziwa ni ya kifantasia 48

3.4 Wakati katika kazi za uhalisiajabu hausongi 51

3.5 Wahusika na uhusika. 52

3.6 Upanuaji wa mwanda wa kisimulizi 55

3.7 HITIMISHO 57

**SURA YA NNE** 58

**UMUHIMU WA SIFA ZA KIUHALISIAJABU KATIKA UTENZI WA MWANA FATUMA.** 58

4.0 UTANGULIZI ........................................................................................................ **58**

4.1.0 Umuhimu wa sifa za kiuhalisiajabu katika kuendeleza maudhui ya kidini. ........................ **58**

4.1.1 Fahari ya watu wa dini ........................................................................................ 58

4.1.2 Kitambulisho cha kidini ........................................................................................ 61

4.1.3 Ukombozi na muungano wa waumini .......................................................................... 63

4.1.4 Ukuzaji wa imani ya kidini .................................................................................... 64

4.1.5 Ruwaza ya kufuatwa kama dini. ................................................................................ 66

4.1.6 Hitimisho ..................................................................................................... 69

**SURA YA TANO ........................................................................................................ 70**

5.0 MAHITIMISHO. ........................................................................................................ 70

5.1 Mapendekezo ........................................................................................................ 72

Marejeleo ............................................................................................................ 74

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Utenzi ni kisa au hadithi ndefu ya kihistoria inayohusu shujaa wa kike au kiume aliyewahi kuishi au anayeaminika aliishi. Aghalabu tenzi hugawika katika mistari minne.Tenzi ni nyingi na hasa katika jamii za Uswahilini. Baadhi za tenzi ni pamoja na *Utenzi wa Howani Mwana Howani na Mwana Kukuwa*, M*wana kupona, Mwana Fatuma, Ukombozi wa Kenya wa Ukombozi wa Zanzibar, Utenzi wa Fumo Liyongo* na nyingine nyingi.

Kimani na Chimerah (2008), wanadai kuwa utenzi ni ushairi wenye mizani chache kuliko kumi na mbili, na ambao mara nyingi hauna vina vya kati katika mishororo, bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake: isipokuwa mstari wa mwisho katika kila ubeti. Kina kinachorudiwarudiwa huitwa bahari. Tenzi nyingi husimulia visa virefu vya kihistoria, hadithi, au mawaidha marefu.

Utenzi kulingana na Wagiriki wa kale hutokana na: neno, hadithi, shairi na ushairi mrefu wa kisimulizi, kikawaida unaohusu mada kuu inayaoshughulikia matukio na shughuli za kishujaa yanayoashiria itikadi au taifa.

Albert na Parry wanadai kuwa tenzi zilizoandikwa mwanzoni zilikuwa katika ushairi wa kimaongezi. Aina nyingine za utenzi ni ya kimhtasari inayosimulia shairi lenye mahaba, lenye neno ambalo lina maana '*utenzi mdogo'* lilianza kutumika karne ya 19.

Tenzi za kwanza zilikuwa masalio ya jamii zisizoelimika na ushairi wa kitamaduni wa kimazungumzo. Katika tamaduni hizi, ushairi uliwasilishwa kwa hadhira kutoka kwa muigizaji kuelekea kwa mwigizaji kupitia katika mazungumzo.

Katika tenzi mara nyingi jagina hujihusisha katika safari zilizo hatari, anakumbana na hali ngumu ambazo wakati mwingine changamoto hizo humrudisha nyumbani akiwa amekengeushwa na hiyo safari. Jagina katika utenzi huonyesha tabia, hufanya miujiza na huwa mfano mzuri wa kuigwa katika jamii ambamo utenzi husika unachipukia. Jagina wengi wa utenzi huwa wahusika wanaojitokeza mara kwa mara katika hadithi za itikadi yao.

Tenzi mara nyingi hujidhihirisha katika dunia nzima inayojulikana hasa itikadi au ulimwengu, ikiwemo mbinguni na duniani, matendo, matukio na safari zinazochukua miaka ambazo mara nyingi huchukua siku au muda mchache kama masaa.

Mhusika mkuu katika utenzi ni kivuli cha ujagina kinachoashiria wazo la itikadi mahsusi ambayo nguvu na uweza humfanya mtu jagina. Mara nyingi udhaifu na kutofaulu kwa jagina huchukuliwa kama nguvu na uweza. Mara nyingi jagina wa utenzi huwa mpiganaji, kiongozi, sehemu binadamu na sehemu Mungu na matendo yake yanajitokeza akiwa safarini.

Sifa za kijumla na utenzi ni kuwa: kimsingi tenzi mwanzoni zilinuiwa kuimbwa au kukaririwa kama muziki, viumbe wasi wa kawaida mara nyingi hujihusisha katika mahusiano na nchi binadamu, utenzi huwa na kupendelea kwa taifa na una kutopendelea nchi, kimsingi utenzi huibuka kwa vipindi vya kuungana na kuzuru, mada ya utenzi hutangazwa katika mishororo ya kwanza ya utenzi ambapo mtunzi humwomba Mungu ampatie nguvu za kiungu kusimuliwa kisa chake. Utenzi wa kweli huwa mrefu na wenye kutukuka mara nyingi mazingira na sehemu za muda zilizotengwa huwa pana, kunakosekana mpaka wa mahali ambapo jagina anajikita kuwa ni pake.

Utenzi mara nyingi huzunguka jagina, kwa kawaida mtu mwenye utaifa au umuhimu wa kusimuliwa. Mara nyingi katika utenzi viumbe wa kiungu hutembelea mtunzi wa utenzi. Kwa mfano katika utenzi wa kikristo "*peponi lost*" inatueleza hadithi kuhusu mashetani na malaika

wanapigana kwa ajili ya nafsi ya binadamu. Watunzi huwachukulia viumbe hawa wasi wa kawaida kama wa kawaida katika dunia ya ushairi.

Utenzi hujitokeza kuwa wakipekee kwa sababu ya jinsi ya kusimulia, matumizi ya kufana ya kimaongezi, wahusika waliojitokeza kikamilifu na hoja muhimu ambazo zinaoana na jamii husika. Tenzi nyingi za Kiswahili zinapatikana katika jamii ya Uswahilini. Tenzi hizo ziliibuka kwa sababu ya athari zilizoletwa na Waarabu walioingia mwambao wa pwani kwa ajili ya biashara. Tenzi nyingi katika jamii ya uswahilini mwanzoni zilikuwa katika hati za kiarabu na baadaye zikatafsiriwa katika kiswahili.

Waarabu walipongia uswahilini walieneza imani ya kiislamu na kwa hivyo watu wengi wa pwani wakawa waumini wa dini ya kiislamu. Tenzi nyingi za uswahili zilihusu mashujaa, ukuzaji wa imani na si imani yoyote ile bali imani ya dini ya kiislamu. Tenzi nyingi zilizotungwa na watunzi zimechukua mwelekeo mmoja, mtindo wa uandishi wa tenzi hizo inaelekea kufanana hata kama maudhui hayafanani.

Katika utunzi, mtunzi hutayarisha vifaa atakavyovitumia katika uandishi wake. Mwanzoni mwa utenzi mtunzi huanza kwa maombi, akimshukuru Mungu kwa kumtunukia nafasi hiyo. Baadaye mtunzi humwombea mtume Muhammad na maswahibu wake kwa sababu kwa kufanya hivyo atapata baraka kutoka kwa mwenyezi Mungu. Baada ya maombi mtunzi huutunga utenzi wake na kuelekea mwishoni mwa utunzi, mtunzi hujitambulisha jina lake na mahali anapotoka.

Tenzi nyingi za Uswahilini zinaangazia maswala ya malezi, maadili, utamaduni na dini. Kwa mfano *Utenzi wa Mwana Kupona*, *Utenzi wa Howana Mwana Howana* na hata *Utenzi wa Mwana Fatuma* zinaangazia kwa kina maelezi ya mtoto wa kike. Mtoto wa kike anafundishwa

jinsi anavyostahili kuishi katika jamii kwa kuwa mwadilifu kwa kila hali. Mtoto wa kike anafundishwa jinsi ya kumtunza mume wake na kumwajibikia.

## 1.1 Tatizo la utafiti

Katika utafiti wetu swala la kiuhalisiajabu katika kuendeleza maudhui ya kidini katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* halijashughulikiwa kwani hatujapata ushahidi wowote. Watafiti walioushughulikia utenzi huu walionekana kuegemea upande wa fani, ujagina, maudhui na maswala ya Mwanamke hasa katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Tumeonelea kuwa watunzi hawa wawili walinuia kuusawiri uhalisiajabu katika kuendeleza maudhui ya kidini. Ni matamanio yetu kuelezea sifa za kiuhalisiajabu katika utenzi huu. Somo hili limeangazia sifa za uhalisiajabu na umuhimu wake katika utenzi huu.

## 1.2 Malengo ya utafiti.

Malengo ya utafiti huu ni :

1. Kuchanganua matukio ya kiuhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.*
2. Kuchunguza namna sifa za kiuhalisiajabu zinavyojitokeza katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.*
3. Kueleza na kubainisha umuhimu wa uhalisiajabu katika kuendeleza dini.

## 1.3 Sababu ya kuchagua mada

Tumechagua kutafitia mada hii kwa sababu zifuatazo: Watafiti waliotafitia utenzi huu waliushughulikia kitofauti. Hii ina maana kuwa uhalisiajabu haujashughulikiwa popote katika tenzi. Wengi wa watafiti wametafitia uhalisiajabu katika riwaya na tamthilia na walikosa

kuelewa kuwa tenzi kama simulizi nyingine zozote zina uhasiliajabu. Hawaamini kuwa ushairi kama utanzu wa fasihi ni usimulizi ambao huwasilishwa kwa njia ya mkato lakini ujumbe hupitishwa sawa na ilivyo katika tanzu nyingine zinavyowasilishwa. Kwa hivyo sisi kama watafiti tumegundua kuwa kuna pengo la nadharia na vile vile pengo limedhihirika katika kazi yenyewe kwa ujumla. Kwa sababu ambazo tumezitaja hapo juu ndizo zilitupelekea kuichagua mada hii. Tumechambua matukio ya uhalisiajabu na umuhimu huu wa uhalisiajabu katika kuiendeleza dini. Pili, tulivutiwa na somo hili la kupambanua sifa za uhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* na umuhimu wake.

Tumetamania kuwa utafiti wetu utakuwa msingi wa kuwaongoza watafiti wa baadaye watakaokuwa na nia ya kuchanganua sifa za uhalisiajabu katika tenzi nyingi nyinginezo. Kwa mfano, inawezekana kuwa sifa za uhalisiajabu katika tenzi nyingine zikawa tofauti na *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Kwa kuchunguza namna sifa za uhalisiajabu zinavyojitokeza katika utenzi huu, kueleza matukio ya uhalisiajabu na umuhimu wake, tunaamini kuwa matokeo ya utafiti huu yatatusaidia kupuuza madai ya watu kuwa uhalisiajabu haupo katika tenzi.

## 1.4 Nadharia tete.

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo.

1 Matukio ya Kiuhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*.

2 Sifa za uhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*.

3 Uhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* una umuhimu mkubwa katika kuiendeleza dini.

## 1.5 Upeo na mipaka.

Utafiti wetu umejikita katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* kwa kuyangazia matukio ya kiajabu, sifa za kiuhaliajabu pamoja na umuhimu wake. Ingawaje bado kuna vitabu vingi vinginevyo vinavyoangazia utenzi huu. Kwetu sisi tumejikita katika maswala maalum. Tumepata kuwa sifa za kiuhalisiajabu zinajitokeza katika utenzi huu. Maswala tutakayoshughulikia ni pamoja na ; matukio ya kiajabu, sifa za kiuhalisiajabu na umuhimu wa uhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.*

## 1.6 Msingi wa Nadharia

Nadharia ambayo tumeitumia katika utafiti wetu ni ya uhalisiajabu. Nadharia hii pia hujulikana kama nadharia ya uhalisia mazingaombwe na ni mojawapo wa nadharia za usasa leo ambazo hushikilia kwamba kazi ya fasihi hujegwa kutokana na mchangamano wa tajriba au uzoevu. Kulingana na Zamora na Faris (1995) nadharia ya uhalisiajabu iliasisiwa mwaka wa 1925 na Mjerumani Franz Roh aliyekuwa mhakiki wa sanaa. Franz ndiye alitumia istilahi ya uhalisiajabu katika muktadha wa sanaa kuelekeza na kuonyesha jinsi ya kusawiri aina fulani ya uajabu kwa mara ya au mazingaombwe yaliyomo kwenye uhalisi uliozoeleka na unaotokana na ujaribati. Kwa sababu ya madai Zamora na Faris nadharia ya uhalisiajabu imetufaa kwa sababu ya yale tumeyashughulikia yanasawiri aina ya uajabu au umazingaombwe.

Mbatiah (2002:60) anaeleza kuwa istilahi hii inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Kulingana na madai ya Mbatia, nadharia ya uhalisiajabu imekuwa ya manufa kwetu kwa sababu katika utenzi huu ni ya kijantasia lakini jinsi yamesawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia na

yanaelezwa kwa njia ya moja kwa moja utafikiri ni mambo ya kawaida Cooper (1998), anadai kuwa hali za kushangaza na kuogofya, huwasilishwa kana kwamba ni hali za kawaida.

Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* kuna hali za kuogofya za kushangaza kwa mfano pale wakati ambapo Ali anapokutana na mtu asiyemjua na anamkopesha ngamia baada ya kuwapa maskini pesa alizokuwa amepata baada ya kufanya kazi anapokuwa anarudi nyumbani. Ali anapokutana na muuza ngamia na anamuuzia kwa deni na baada ya mwendo si mrefu anakutana na mnunuzi ambaye anampatia pesa zaidi na vile anatarajia. Kwa maelezo hayo tunaonelea kuwa nadharia ya uhalisiajabu imetufaa na kutuwezesha kupata matokeo bora.

Wamitila (2004) anamuunga Mbatiah kwa kudai kuwa dhana ya uhalisiajabu huhusishwa na Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa ulimwengu wa tatu. Sifa yake kuu ni kuyaeleza matukio ya kifantasia au ya kiajabu ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa maana inayoyafanya yaonekane ya kawaida. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha kuwa matukio aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika . Maelezo yake kuhusu nadharia ya uhalisiajabu yanatuwezesha kuitumia nadharia hii katika kazi yetu kwa sababu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* mtunzi wa utenzi huu ameyaangazia matukio ya ki ajabu kwa namna ya moja kwa moja na ameyafanya yaonekane ya kawaida. Tumepata kuwa mtunzi ametumia mtindo huu kuonyesha kuwa matukio husika yanapatikana katika maisha yas kawaida.

Wamitila (2008) anadai kuwa huwepo matukio ambayo ni vigumu kuyaelezea katika msingi wa uhalisi wa kawaida katika jamii. Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* mtunzi ameangazia matukio ambayo ni vigumu kuelezea katika msingi wa uhalisia wa kawaida kwa mfano maandalizi ya harusi ya Fatuma kule mbinguni ambapo malaika wanafanya maandalizi hayo.

Alexander (1990:127) anasema kwamba, uhalisiajabu ni kielelezo cha jinsi nadharia ya usasa leo inavyotulazimu kufikiria upya juu ya riwaya za kimapokeo kuhusu riwaya za uhalisia za karne ya kumi na nane na tisa. Roh (1925) alitumia neno uhalisiajabu katika muktadha wa ulimwengu wa sanaa kueleza aina fulani maalum ya kudhihirisha usiri ulioko kwenye maisha ya kila siku bila kuupigia maswali yoyote uhalisia huo. Pamoja na hayo uhalisiajabu katika kazi ya sanaa hushughulika na kazi zinazoambatana na zisizoambatana na ujumi wa uhalisia.

Chanady (1985) katika Rio (1999) anasema kwamba uhalisiajabu unahusu matukio yasi ya kawaida, ya kiujiza au chochote kilicho kinyume cha uhalisia wa kawaida. La muhimu zaidi ni kwamba matukio yanayotendeka katika uhalisiajabu hayawezi kujitenga na uhalisia. Matukio yasiyo ya kawaida,s ya kiujiza na ni kinyume cha uhalisia wa kawaida.Vilevile nadharia ya uhalisiajabu imekuwa ya muhimu zaidi kwa sababu Chanady anasema kuwa la muhimu zaidi na uhalisiajabu ni kwamba matukio yanayotendeka hayawezi kujitenga na uhalisia.

Msingi wa kinadharia  Okah (2002: 94) akizihakiki kazi za Okri (1991) anasema kuwa katika uhalisiajabu, uhalisia na ndoto havitofautishwi. Kuhusiana na haya maelezo yake, nadharia hii imestusaidia katika uchambuzi wa kazi yetu kwa sababu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* ni vigumu kwa msomaji kutofautisha uhalisia na ndoto.

Waandishi wa uhalisiajabu ni pamoja na E. Kezilahabi, W. Mkifya, E. Mbogo,  K.W Wamitila na S.A Mohamed ambao wametumia uhalisiajabu katika uwandishi wao kazi za riwaya na tamthilia kwa njia ya kuendeleza maudhui ya ukoloni na adhari zake. Kazi zilizo shughulikiwa na S.A Mohamed katika kipindi cha uhalisiajabu ni kama vile: *Pungwa (1988), Kivuli kinaishi (1990)* na *Amezidi (1995)*. Ingawaje wao wametumia uhalisiajabu katika tamthilia na riwaya kuendeleza maudhui ya ukoloni, kazi hii imetufaa katika kazi yetu kuendeleza maudhuiya kidini na umuhimu wake.

Nadharia ya uhalisiajabu inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyozoeleka na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ya ishirini. Matukio yasiyoaminika na ya kifantasia husawiriwa, mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja kuonekana kana kwamba ni ya kawaida. Kwa hivyo hii ndiyo nadharia mwafaka katika uchambuzi wa kazi yetu kwa sababu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* ambapo kuna matukio yasiyoaminika ya kifantasia yanasawiriwa kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni ya kawaida. Vilevile mambo ya kiajabu yanaelekezwa kwa namna ya moja kwa moja kana kwamba ni ya kawaida.

Rogers (2002) anaeleza kuwa uhalisiajabu hujaribu kuwasilisha mojawapo wa au kadhaa wa uhalisia wa mwonoulimwengu ambao kwa hakika upo au uliwahi kuwepo. Uhalisiajabu ni mojawapo ya uhalisia lakini moja tofauti kutoka kwa uhalisia ambao tamaduni zetu nyingi zinakumbwa kwa sasa. Maelezo ya Rogers kuhusu uhalisiajabu ni ya manufaa kwani yanatupatia mwelekeo katika kutumia uhalisiajabu kama nadharia.

Maelezo kulingana na mtandao ni kuwa uhalisiajabu ni hali ambapo hali zisizo za kawaida zinachukuliwa kama za kawaida katika mazingira ya kawaida. Ingawaje uhalisiajabu unachukuliwa kama wa kifasihi vilevile unahusishwa na filamu na sanaa ya utazamaji. Mfano ya uhalisiajabu unadhihirika pale mhusika katika kazi ya kifasihi anaendelea kuishi zaidi na matarajio ya umri wa kawaida. Pia uhalisiajabu unajitokeza pale mhusika huyo anaishi katika vizazi vingi. Kwa juu juu kazi ya fasihi haina uhalisia ajabu wa moja kwa moja na kwa hivyo kila kitu kinawasilishwa kwa njia ya kawaida na ya moja kwa moja ingawaje mhusika kama huyu huvunja mipaka ya uhalisia wa kawaida. Maelezo haya ni muhimu kuhusu nadharia ambayo tumetumia  katika kazi yetu.

Strecher (1999) anafafanua uhalisiajabu kama ‘kile kinachotendeka wakati ambapo ukweli wa ndani wa mandhari ya juu unapoingiliwa na kitu ambacho ni cha kiajabu sana

kuaminika’. Mtazamo huu wa uhalisiajabu unatokana na usomi wa watu wa nchi za Magharibi kutohusishwa na imani ambayo ni mzizi wa uhalisiajabu ambao ni rahisi sana kueleweka na tamaduni za watu wasi wa Magharibi. Mawazo ya Strecher yametufaa katika utafiti wetu kwani yanatuwezesha kuielewa nadharia ya uhalisiajabu kwa kina. Uhalisiajabu hutumia mbinu za kifasihi simulizi ambazo ni uajabu, umazingaombwe na ufantasia kuonyeshwa kuwa kawaida.

**1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Somo.**

Udurusu wetu wa yaliyoandikwa kuhusu somo hili umejikita katika ushairi wa Kiswahili na hasa mashairi ya kale (Mashairi yaliyoandikwa kabla ya karne ya ishirini). Tumeamua kuchukua msimamo huu kwa kuwa tenzi nyingi za kidini ziliandikwa wakati huo. Katika durusu zetu tumegundua kuwa uhalisiajabu umeshughulikiwa katika riwaya na tamthilia na wala si katika tenzi.

Nyambunga (2005) ameshughulikia uhalisiajabu katika riwaya ya *Musa Leo* na *Babu alipofufuka* katika tasnifu yake ya uzamili sawa na Maganju (2004) aliyeushughulikia uhalisiajabu katika riwaya ya *Babu alipfufuka* na *Bina-Adamu!* katika tasnifu yake ya uzamili. Watafiti hawa wawili wameshughulikia sifa za kiuhalisiajabu katika riwaya. Ingawaje kazi yetu inahusisha uhalisiajabu katika utenzi kazi zao zimetufaa tulipochambua sifa za kiuhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Tunapata kuwa wameweza kuyaangazia matukio ya uhalisiajabu katika kazi zao. Hili limetusaidia kwa kiasi kikubwa kwa sababu baada ya kupitia kazi zao tumeweza kuelewa zaidi jinsi ya kuyateua matukio ya kiuhalisiajabu kutokana na kazi yetu.

Wamitila (2008) ameshughulikia swala la uhalisiajabu katika riwaya ambapo anaeleza kuwa riwaya ya uhalisiajabu huingiza sifa ambazo zinafahamika na wasomaji. Ametoa mifano

katika riwaya mbili ambapo ni vigumu kueleza jinsi Munene anavyofukuzwa na fuvu katika *Dharau ya Ini* au jinsi Kakulu anavyoweza kuongea, kutania watu na kukimbia mara tu anapozaliwa katika *Mzingile.* Matukio ya kiajabu katika *Dharau ya ini* na *Mzingile* ni muhimu katika utafiti wetu kwani kupitia kwayo imetusaidia kuelewa zaidi juu ya matukio ya kiajabu ambapo wakati tulipokuwa tukichambua kazi yetu ilikuwa rahisi kuteua matukio ambayo si ya kawaida jinsi ambavyo Wamitila ameweza kufanya. Kwa hivyo kazi ya Wamitila ilitufaa zaidi.

Tamthilia ya *Pungwa* imeangazia migogoro kati ya mapepari na wafanyikazi nayo thamthilia ya *Kivuli kinaishi* imeangazia misingi ya kiimla na jinsi inavyoendelezwa kwa njia ya ukandamizaji, uwongo na ufisadi. Wafula (1999) anasema kuwa dalili za uhalisia ajabu zinaonekana katika tabia ya Kirembwe ambaye anajilinganisha na kati ya miungu wa Roma pale anajipa uwezo na sifa za kuishi daima; vilevile anasema kwamba kuzaliwa kwa Kirembe kulifumwa katika miujiza. Hizi hali zote zinadhibitisha uhalisiajabu.Ingawaje kazi hii ni ya tamthilia itatusaidia katika kuchanganua sifa za kiuhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana na Fatuma* kwani kuna hali na matukio ya kiajabu kama yanayoangaziwa katika tamthilia hizo ndiyo yanayodhihirika katika utenzi huu kwa hivyo kazi hii ilistufaa zaidi.

*Amezidi (1995)* ni tamthilia iliyo na matukio ya kiajabu kwa mfano kuna wahusika wanaokufa kwa kipindupindu baada ya kula nyama ya msaada iliyooza. Ame na Zidi wanaishi kwenye' kasri' lakini wanapokaribia kufa hawana hata tone la maji la kukata kiu walichokuwa nacho. Kasri wanamoishi ni la mawazo, wanapiga simu zisizo kuwepo na kulalia vitanda vipana vya kufikirika tu. Kwa sababu matukio katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* ni ya kufikirika kazi hii imetufaa.

Topan, katika tamthilia ya *Aliyeonja Pepo (1973)* na Hussein katika tamthilia ya *Mashetani (1971)* wanakaribia kutumia mbinu za uhalisiajabu ambapo wanachota mitindo yao

kutoka katika malighafi ya fasihi simulizi ambapo tangu kale dhana ya miungu, mashetani, pepo na mengine zimekuwepo. Kezilahabi ni mwandishi na Mwanafasihi mwenye umahiri wa kutumia mtindo wa uhasiliajabu. Mbatia (1997) anasema kuwa katika *Nagona* na *Mzingile* za E. Kezilahabi, mwandishi anamsafirisha msomaji kutoka mazingira ya kiulimwengu aliyoyazoea na kumpeleka kwenye ulimwengu wa kindoto baina ya kifo na uhai, kuwa macho na kuwa ndoto.

Mohamed (2001) na Wamitila (2002) wanatumia uhalisiajabu katika uandishi wao kimaksudi kwa sababu ya kutaka kuyaangalia maswala ya kijamii kiajabu na kwa njia ya kipekee. Topan, Hussein na Kezilahabi wanafahamika zaidi kwa kuzingatia uhalisiajabu. Kwa ajili ya kutumia uhalisiajabu katika uandishi wao, kazi zao zimetufaa kuelewa zaidi juu ya matukio ya uhalisiajabu na sifa zake jambo lililotusaidia katika utafiti wetu.

Hauge (1974) ametalii dini, utamaduni, imani, itikadi, miiko, mahusiano ya Wajaluo na Mungu wao, wafu na mambo mbalimbali kuhusu Wajaluo. Vilevile anatuelezea kuhusu historia ya Wajaluo na hadithi mbali mbali kuhusu watu wao maarufu kama vile watabiri, waganga, waponyaji, wanasiasa na hata wengine waliotenda mambo ya kiajabu kama vile Joshua Rume na Mien Olando. Hii kazi ilitufaa katika utafiti wetu tulipoangazia matukio na sifa za kiuhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Matukio ya kiajabu ya Joshua Rume na Mero Olando yalituwezesha kuyachanganua matukio ya kiajabu katika utenzi husika.

Olali (2006) alishughulikia uhalisiajabu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*. Olali anadai kuwa mwandishi wa riwaya hiyo ambaye ni Mohamed anatumia majaribio na uhalisiajabu kwa mara ya kwanza. Anasema kuwa uhalisiajabu katika riwaya hii unatokea pale kunazuka mzuka mara kwa mara katika kasri la K, katika gari lake na njiani anapoendeshwa na dereva wake.

Olali (2006) anasema kuwa Ahmed Mohamed anatumia sifa za kiuhalisiajabu kuonyesha kuwa shughuli kama zile hutokea katika hali halisi na katika mazingira ya Uswahilini.

Hata kama kazi ya Olali ilihusu riwaya imetufaa katika utafiti wetu kwa sababu ameeleza sifa za kiuhalisiajabu kulingana na Wamitila. Sifa hizi ndizo zimestufaa kwa kiazi kikubwa zaidi katika kazi yetu ya utafiti. Vilevile Olali ameeleza jinsi ambavyo uhalisiajabu unavyojitokeza katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* kwa kutaja matukio yanayozua uhalisiajabu. Bado kama watafiti tunaona kuwa mifano ya matukio ya kiajabu iliyoangaziwa ilitufaa katika kuchambua matukio ya kiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Kwa hivyo tunaona kuwa kazi ya Olali imekuwa ya manufaa na yenye mchango mkubwa katika utafiti wetu.

Mwandishi wa riwaya ya *Kusadikika* Shaaban Robert ameusawiri uhalisiajabu pale ambapo Mfalme Jeta ana uwezo wa kumeza chochote apatacho na kuwa hata baada ya kula kwa pupa, yeye mfalme Jeta hashibi kwa vyovyote vile. Ingawaje mwandishi huyu ameusawiri uhalisiajabu katika riwaya, kazi yake ilikuwa ya manufaa kwetu sisi kama watafiti kwa kuwa huo uhalisiajabu unaopatikana katika matukio ya kawaida na yale yasiyo ya kawaida katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.*

Katika tamthilia ya *Kinjeketile* ya Hussein ameuhusisha uhalisiajabu katika maelezo yake katika vita ambavyo Wakerewe wanapigana na Wajerumani wanapotafuta ukombozi wao. Kinjeketile ambaye ni kiongozi wa Wakerewe anajifanya kuwa ana uhusiano wa karibu sana na miungu na kuwa Mungu anamtumia ili awakomboe Wakerewe. Inadaiwa kuwa kuna wakati anatumbukia ndani ya maji na wakati wa kutoka majini nguo zake hazilowi maji.

Kwa hakika hili si jambo la kawaida mtu kiingia majini na atoke nguo zake zikiwa zimekauka. Lakini mwandishi wa tamthilia amelisawiri tukio lisilo la kawaida kuonekana ni jambo la kawaida. Kazi hii imetufaa kwa sababu utafiti wetu umechanganua uhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Hata kama kazi hii ni tamthilia imetufaa sisi kama watafiti wa uhalisiajabu kwani tumeyaangazia matukio ya kiajabu katika utenzi huu.

Mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Issa* Musa Mzenga ameutumia uhalisiajabu kwa kiasi kikubwa sana. Uhalisiajabu katika *Utenzi wa Nabii Issa* umetumika kwa kiasi kikubwa katika kuwasilisha maudhui ya kidini. Kuna matukio mengi sana katika utenzi huu ambayo katika hali ya kawaida, binadamu wa kawaida hawezi kukubaliana nayo. Lakini mtunzi anayaangazia na kuyasawiri kana kwamba hakuna lolote la ajabu kwani haya ni matukio kama ya kawaida kulingana naye. Ni baada ya msomaji kuyasoma matukio hayo ndipo anashangaa na kazi ya Musa Mzenga. Kazi ya Musa Mzenga ni ya manufaa makubwa sana kwa sababu tumeona kuwa nia ya mtunzi huyu ni kuendeleza maudhui ya kidini. Kwa sababu hiyo *Utenzi wa Nabii Issa* umetufaa sana kwani umetuelekeza katika kuyachunguza matukio ya kiajabu na yanayochangia pakubwa kuendeleza maudhui ya kidini.

*Biblia Takatifu* imeutumia uhalisiajabu katika kuuwasilisha ujumbe wa kuiendeleza na kuikuza imani ya waumini wa dini ya Kikristo. Kwa mfano katika kitabu cha Mwanzo ambapo tunaambiwa kuwa kila kitu kiliumbwa kiajabu yaani Mungu anatumia maneno na hayo maneno yanasababisha kuweko usiku na mchana, nchi kavu na mito, mbingu na ardhi, wanyama na mimea, na hata mtu wa kwanza duniani anaumbwa kwa mfano wao. Mungu anasema ‘Na tumuumbe mtu kwa mfano wetu’. Uajabi zaidi ni pale ambapo Mungu ni pekee yake lakini anasema kuwa wamuumbe binadamu kwa mfano wao pale wao ni Mungu, Mwana na Roho Mtakatifu.

Mifano zaidi katika Biblia ni pamoja na Musa kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri ambapo Musa anatumia fimbo kutawanya maji ya bahari ya Shamu, maji yakagawanyika na katikati kukawa na ardhi kavu ambapo Waisraeli wanapita na Wamisri wote wanakufa. Vilevile uhalisiajabu unadhihirika katika kuzaliwa kwa Yesu Kristo pale Maria anatokezewa na malaika kuwa atamzaa Mwana bila ya kuonana na mwanamume, jambo ambalo si la kawaida. Katika

kitabu cha Danieli inadaiwa kuwa Danieli alitupwa kwenye tundu la simba akalala ndani usiku kucha na anatolewa akiwa hana jeraha lolote. Jambo hili si la kawaida lakini katika Biblia linachukuliwa kama la kawaida. Mfano mwingine ni wa Meshaki, Shadraki na Abednego wanapotupwa kwenye tanuru ya moto na badala ya watu watatu kuwa motoni kunakuwa na watu wanne ambapo mtu wa nne anadaiwa kuwa ni Yesu Kristo. Ajabu zaidi ni kuwa hawachomeki na hata wanapotolewa motoni mili yao inabaki jinsi walivyorushwa motoni bila hata harufu ya moshi. Mifano zaidi ni Yesu kutengeneza divai katika harusi, Yesu na Petero kutembea Juu ya Maji, Hagari mamake Ishmaeli anaelekezwa palipo maji jangwani, Yesu kuamuru mawimbi kusita baharini wakati chombo cha usafiri kinapoelekea kuzama, Elisha kulishwa na kunguru.

Matukio ya kiajabu yanayojitokeza katika Biblia yatatufaa katika kazi yetu kwa sababu tunapata kuwa hayo matukio yote ni ya kuendeleza maudhui ya dini ya Kikristo. Kwa hivyo matukio haya yametuelekeza kuyachambua na kuyachanganua matukio ya kiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* ambao ni wa kidini unao endeleza maudhui ya dini ya Kiislamu. Kwa hivyo Biblia imetufaa katika kazi yetu ya utafiti.

Esquivel katika novela ya *Like water for Chocolate* ameeleza juu ya mwanamke anayeishi maisha ya kutengwa. Mhusika mwanamke kwa jina Tita ananyimwa haki yake ya furaha na ndoa na mama yake. Hali hii inamwelekeza kutafuta nguvu zisizo za kawaida za kurithisha hisia zake na kwa hivyo nguvu zisizo za kawaida zinatokana na chakula anachokipika. Wanaokila chakula chake wanarithisha hisia zake.  Kwa mfano anayeionja keki ya harusi iliyopikwa na Tita kutokana na pendo lisilokubaliwa. Wageni waalikwa wote hukumbwa na wimbi la kutaka au kutamani kupenda.

Morrison (2004), katika kazi yake ya ‘ *Beloved’* anaeleza hadithi juu ya mama ambaye anapagawa na mzuka wa mwanawe, anaibua mbinu za kuishi na kukubali fikra zake za mara kwa mara za utotoni anapodhulumiwa kama mtumwa na mzigo wa kuwakuza watoto katika jamii katili. Kazi hii ya Morrison imetufaa katika utafiti wetu hata kama inahusisha riwaya. Matukio ya kiajabu anayoifafanua ndiyo yametusaidia katika kuyachanganua matukio ya kiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*.

Silko (1977), katika kazi yake ya *‘Ceremony’* kwa mfano kuna tukio pale ambapo mwanamke anacheza kwa hasira. Mbali kutoka na pale anapochezea Mwanaume aliyemsaliti anachunga ng’ombe wake ambao wanapigana. Mikanyago ya miguu ya kucheza kwa huyu mwanamke inaenda sambamba na mikanyago ya kwato za ng’ombe hao ambao wanamkanyaga na kumuuwa mwanamume. Ukweli unaojitokeza ni kuwa mwanamke anaweza kukasirika na kwamba anapocheza, mume wake anakufa. Kazi hii imetufaa katitka utafiti wetu kwa sababu imehusisha uhalisiajabu ambao unapatikana katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.*

**1.8 Njia za utafiti.**

Tumesoma kwa kina *Utenzi wa Mwana Fatuma* na kazi nyingine. Tumesoma miswada inayohusiana na utenzi ukiwemo mswada wa Ernst Dammann wa *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Tumezisoma tasnifu za watafiti wengine waliotutangulia hasa waliotumia nadharia ya uhalisiajabu kupata njia ya kulishughulikia swala letu la utafiti. Kwa sababu *Utenzi wa Mwana Fatuma* umeandikwa katika mtazamo wa dini ya Kiislamu tumevisoma vitabu vilivyotusaidia kuelewa *Utenzi wa Mwana Fatuma.*

## 1.9 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia maswala ya kimsingi yanayohusiana na utafiti huu. Maswala haya ni pamoja na: utangulizi, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, nadharia tete, upeo na mipaka, Msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu somo na njia za utafiti zilizotumiwa.

# SURA YA PILI

## MUHTASARI WA *UTENZI WA MWANA FATUMA* NA MATUKIO YA KIAJABU.

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia mukhtasari wa *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Tumeangalia jina la mtunzi na wakati utenzi ulipotungwa. Pia tumetaja mahali utenzi ulitungiwa. Baada ya maelezo hayo tumechanganua *Utenzi wa Mwana Fatuma.* Baadaye tumechanganua matukio ya kiajabu yanavyojitokeza katika huu utenzi. *Utenzi wa Mwana Fatuma* ulitungwa na Binti Said Amin Bin Uthman aliyeishi kati ya mwaka 1800 na1900 ambaye aliishi katika kisiwa cha Lamu katika Pwani ya Kenya.

Kimani na Chimera (2008) wamedai kuwa ushairi ni sanaa ya lugha inayoeleza jambo au wazo kwa njia ya mkato, na kwa namna inayoteka hisia za msomaji au msikilizaji.Wanaendelea kudai kwamba ushairi ndio utanzu mkongwe zaidi katika jamii za kilimwengu. Ulianza wakati binadamu alipobuni lugha; jambo ambalo lilimtoa mtu katika hali ya uhayawani na kumfanya kiumbe razini. Mabadiliko haya yalimfanya mtu ayaelewe mazingira yake na aweze kutoa mchango wake katika kuyakabili na kuyabadilisha. Ubunifu wa lugha na uzalishaji mali ulishajiishana kwa kuwa maneno yalitokana na shughuli za kizazi au umilikaji wa mazingira.

Wamitila (2002) anadai kuwa baadhi ya tungo ambazozinaelezwa kama zilitungwa wakati fulani, huenda zilikuwa zikikaririwa au kupokezanwa kwa njia ya mdomo na hatimaye kuiashia kuandikwa wakati huo unaosemwa. Anapeana, mfano wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* uliotungwa na Mohamed Kijumwa katika mwaka wa 1913, lakini zipo sababu nyingi za kutuwezesha tuamini kuwa kulikuwako na utendi simulizi kuhusu Fumo Liyongo kabla ya wakati huu.

Imedaiwa kuwa utungo wa kwanza wa kishairi ni *Hamziya,* ambao ni utungo wa kikasida unaomsifu Mtume Mohammad. Utungo huu unasemekana ulitungwa mwaka wa 1652 au hata kabla na ni tafsiri ya utungo wa *Karibu Umma Ul Qura (Mama wa Miji)* wa mshairi wa Ki-Sufi kutoka Misri. *Sifa za Mwana Munga* /*Utendi wa Mwana Munga*, ndio wa zamani sana na ulitungwa mwaka wa 1517. Swala la tarehe limezua utata kwani mpaka leo ithibati ya kihistoria ya kutegemewa kuhusu alipoishi Liyongo. Wasomi wengi wanaelekea kuamini kuwa Fumo Liyongo ni msingi mkuu wa kuchunguza historia ya ushairi wa Kiswahili.

Baadhi ya tungo za zamani za fasihi ya Kiswahili ni pamoja na *Utendi wa Mwana Munga*, *Hamziya, Utenzi wa Tambuka, Utenzi wa Vita vya Badri, Utendi wa Ayubu, Utendi wa Mikidadi na Mayasa, Sir ili Asirari Ayi Wangiwangi, Utendi wa Qiyama, Kasida ya Burudai,Al-Inkishafi, Shamiuni*, *Dua*, *Dura Mandhuma*, *Ukawafi wa Miraji, Utendi wa Haudaji, 'Takhmisa ya Liyongo'*, *Utenzi wa Shufaka,' Shauri la Makunganya'.*

**2.1. Mazoea ya Mtunzi**

Katika ubeti wa kwanza hadi ubeti wa sita, Mtunzi anaagiza vifaa ambavyo ananuia kuvitumia katika uandishi wa utenzi wake. Katika kujitayarisha katika uandishi wake wa utenzi katika sehemu hii ya utangulizi tunaona kuwa hayo ni matayarisho pale mtunzi anaitisha kalamu, wino na karatasi Mtunzi anasema kuwa uandishi uwe mzuri ndiposa macho yaweze kusoma. Baada ya kuletewa kila kitu anachotarajia kutumia katika uandishi wake ndipo mwandishi anamwomba Mungu mwenyezi asiye na mshirika yeyote.

### 2.2 Maombi, sifa za Allah na maajabu ya uumbaji

Katika sehemu hii mtunzi anamwomba Allah na kumsifu kwa kuwa ni muumbaji na kumwombea Mtume baraka ambaye ni Mfalme wa Arabia na kuwa Mungu alimfanya kuwa Mwombezi. Anaeleza kuwa Mungu alimfanya kuwa Mfalme mwenye uwezo, anayeumba na kuharibu na anayeeneza uwezo wake juu ya kila mmoja. Mtunzi anaeleza kuwa falme mbili, ule wa juu na wa chini ni za Mungu, Peponi na malaika, muumba ni mtakatifu na kuwa hakuna yeyote anayeweza kupinga au kukataa kwa kuwa kila kitu kinachotajwa kwa kila mwanadamu anayetajwa na mbingu zinazotajwa kuna mmoja tu aliyeumba. Anaeleza kuwa ardhi na mbingu nyota kubwa na ndogo na kila kitu kilicho na uhai aliyeumba ni mtakatifu.

Mtunzi anaendelea kuutaja ukuu wa Mungu anapotaja kuwa malaika na bahari, wanyama wote na ardhi kavu viliumbwa na Mungu ambaye hawezi kulinganishwa na kiumbe mwingine. Anataja simba, ndovu, chui na nyoka wakali, viumbe wanaopaa ambao ni panzi na nzi pia. Aliumba mwezi, wanyama wa baharini, mawingu angani ambayo aliyaweka pamoja.

Miujiza ya Mungu inatajwa zaidi kwa kuwa ni muumba wa viumbe wote, majini, shetani aliyelaani wanadamu, juju wa majuja, mpinga Kristo na hata kama watajiinua juu, wote ni viumbe wake. Kwa ufupi, mtunzi anaeleza ukuu wa Mungu na jinsi ana uwezo juu ya kila kitu ulimwenguni na mbinguni.

Mwishoni mwa sehemu hii mtunzi anahimiza kuwa kila mmoja awe mtiifu kwa Mungu usiku na mchana na aepuke kutenda uovu na aeneze mazuri. Anawashauri wasomaji kuwa, mahakimu wapate baraka na kuwa wachague dini nzuri itakayowawezesha kufa wakiwa waumini na kijiepusha na ushawishi wa shetani.

### 2.3 Sifa za Mtume Muhammad

Mtunzi katika sehemu hii anamsifu na kumtukuza Mtume na anasema anafanya hivi usiku na mchana ili apate fadhila. Anamsifu Mtume ili aweze kuwasilisha ujumbe wake kwa usahihi. Anataja kuwa Mtume Muhammad ndiye wa kwanza kuumbwa kabla ya mitume wengine.

Yeye ni mwangaza, nuru ya Mtume ndiyo iliyokuwa ya kwanza kuumbwa na ikawa na mwanga mkubwa uliowekwa na ukabakia hivyo kwa miaka mingi. Ni kutokana na nuru ya Mtume Muhammad ndipo kila kitu kikaumbwa, yaani falme zote, akili na mwezi vilitokana na nuru ya Mtume Muhammad. Hata kalamu na karatasi ambavyo ni vifaa anavyonuia kuvitumia viliumbwa kwa utaratibu na mwenye nuru ambaye ni kama taa. Kwa hivyo Mungu ni muumba na mwenye utaratibu.

Mtunzi anamtaja Mtume Muhammad kama mwenye baraka, mzaliwa wa Maka na aliyezipanda mbingu saba, Mtume Muhammad ni mwenye ukuu, kupitia kwake watu huomba na hata malaika mbinguni huomba daima. Ni kupitia kwa Mtume, malaika huomba bila shaka kwa sababu yeye ndiye ana uwezo. Mtunzi anasema daima Mtume Muhammad aombewe mchana na usiku daima kwa sababu ni amri ya Mola, kuomba kwa ndimi bila mioyo kuchoka. Mwombezi aombewe kwa kuwa mstari wake uko katika Kurani Tukufu kwa uwazi na kuwa usomwe na kueleweka bayana. Mistari wenyewe ni;

> kauluhu ta ’ala ’inna llaha wa-mala
>
> ’kitahu Yusiwalluna ’ala l-nabiyyi. Ya’ayyuha llazina amanu. Sallu ‘alaihi wa-sallimu tasliman.
>
> Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini!
>
> Msalieni na mumsalimu kwa salamu (Surah 33, 56) (ub. 42).

Mtunzi anaeleza kuwa Muhammad ni Mtume wa Mungu ambaye ni muumbaji na kuwa yeyote asiyemwaamini ni kafiri. Hata kama Mtume ni binadamu, si binadamu wa kawaida kwani mbele ya Mola Karimu hakuna wa kulinganishwa naye. Anasema kuwa Mtume ni mtu mwenye upendo aliyeweka msingi wa haki na kuwa yeye ni muumini na msomi asiye na lawama yoyote. Yeyote asiyemwamini Mtume ni kafiri na makao yake ni motoni. Yeyote anayemkana Muhammad pamoja na mashahidi wa Mungu aliowatuma watahukumiwa. Mungu ametuma aya ijulikane kwa watumishi wake kuwa ataeneza maana yake kwa kumwamini Mtume. Aya anayoishusha Mungu ni juu ya kushuhudia juu ya mteule kuwa ni Mtume wa Mkuu. Aya aliyoituma Mungu ni:-

> ‘kauluhu ta’ ala: ma kana Muhammadun ‘aba ‘ahadiri min rijalikum walakin rasula ilahi’
>
> Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu (surah 33, 40a) (ub. 50).

**2.4 Maudhui ya utenzi na vinne bora**

Mtunzi amesimulia hadithi kumhusu Fatuma bintiye Mtume Muhammad aliyezaliwa katika wema. Anaeleza kuwa, atashughulikia ndoa ya Fatuma, alipoolewa na Ali ambaye ni hodari na jasiri katika vita. Mtunzi anavitaja vitu vinne vinne au viumbe wanne wanne na kati yake anakuwa na kimoja au mmoja bora. Anadai kuwa Mungu aliviumba viumbe wanne na kuchagua kimoja kati yavyo. Aliwaumba malaika wengi zaidi akachagua wanne, ambao ni; Mikaili na Israfili aliye na sifa ya kuchanganyikiwa, malaika wa nne ni Iziraili anayefanya kazi nyingi ya kuzichukua roho za watu.

Mungu aliteremsha vitabu vingi vikubwa vijulikanavyo na vyote vilipokuwa vimetosha alichagua vinne ambavyo ni: Taurati, Injili na Zaburi na Kurani Tukufu. Mitume walioumbwa na Mungu walikuwa wanne ambao ni: Ibrahimu, Musa aliyetumwa na Mungu na Yesu mwanawe Mariamu ambaye ni roho mtakatifu wa Mungu na wa nne ni Muhammad ambaye ni mtulivu anayependwa na Muumba aliyekabidhiwa huduma ya uombezi. Aliwachagua waandamanaji wenye haki ambao ni: Abubakari Sadiki na Umari Faruki, wa tatu inasemekana kuwa ni Saidi Usmani aliyeinakili Kurani kutoka kwenye mifupa ya ngamia na wa nne ni Ali, mkwe wake Mtume Muhammad. Yeye ndiye mkuu na mwenye nguvu kati ya wote kwa kuwa alipigana na kuwashinda simba na kiboko.

Mungu aliumba mharibifu wa makafiri wabaya ambao pahali walipokusanyika na kukaa aliwainua juu kwa kuwatawanya. Aliumba milima mingi akachagua minne ambayo ni Mlima Kafu, Mlima Sinai, Mlima Uhudi na mlima wa nne ambao ni mashuhuri ni Arafia. Mungu akaumba miezi na kuihesabu ikawa kumi na miwili. Baadaye alichagua miezi minne na kuitenga kuwa ya Nabii Muhammad ambayo ni Mfungoni, Rajabu, Shabani na wa nne ni Ramadhani ambao unajumuisha siku zenye neema.

Mwezi wa Ramadhani ni mwezi ambao maombi mengi hujibiwa na matamanio ya watu kutimizwa. Dua za wakati huu huondoa tashwishi yoyote. Kuna Ijumaa na siku mbili za sherehe na ya nne ni siku ya kuriji. Baada ya kuumba siku aliumba usiku akachagua usiku nne nzuri ambao kwanza usiku wa Hijia usiku wa sikukuu mbili za Iddi na usiku wa Mi-raji ikija. Vilevile Mungu aliwaumba wanawake jasiri ambao kati yao aliwachagua wanawake wanne ambao ni: Hawa mama wa ulimwengu mzima, wa pili ni Sarah, wa tatu ni Mariamu naye wa nne ni Jua ambaye ni bintiye Mtume ambaye ni mama yake Hassani wawili (Huseini na Hassani).

## 2.5 Fatuma kama kielelezo bora cha wanawake wote ulimwenguni

*Utenzi wa Mwana Fatuma* unamwangazia Fatuma binti yake Mtume Muhammad pale mtunzi anacheza jinsi ambavyo Fatuma alivyokuwa msichana mrembo asiye na mfano. Uso wa Fatuma uling'aa kuliko mwezi na kuwa yeyote anayemwona alitosheka kwa kuwa aliumbwa akaumbika. Inasemekana kuwa anawashinda bikira wengine kwa mengi hasa katika urembo na uwezo hakuna anayemfikia. Inasemekana kuwa Fatuma alipendwa na babake, ambaye ni Mtume Muhammad na kuwa hangeondoka popote Fatuma alikuwa. Wakati wowote Mtume Muhammad alienda msikitini na kurudi nyumbani Fatuma alimlaki babake. Mtunzi anasema kuwa wakati angetaka kwenda popote alimwita Fatuma ambaye angeruka juu na kumkimbilia baba yake. Wakati Mtume angemwona Fatuma angemwombea na kumwombea msamaha kwa Mungu.

Fatuma anapovunja ungo anaendelea kuwa mrembo na wa kuheshimika na kuwa uso wake uling'ara kama nuru ya jua jambo ambalo linampatia Mtume Muhammad wasiwasi kila wakati. Mtume Muhammad anatamani sana kumjua mkwe wake, ambaye atamwoa binti yake Fatuma ingawa anamngojea malaika Jibrili atoe mwelekeo. Urembo na uzuri wa bikira bintiye Mtume unaenea kote kwa ghafla unaenea Magharibi na Mashariki.

Sifa za Fatuma zilienea kote Uarabuni na zikakita mizizi Misri na I-yaman, na kwa Imamu wa Siria. Kila pembe ya Uarabuni ilipata ujumbe juu ya sifa za urembo na uzuri wa Fatuma binti yake Mtume Muhammad. Vilevile hizi sifa zinaenea Uswisi, Damasiki, Basara na Iraki hadi Kaisaria na Himaya. Sifa za urembo na uzuri wa Fatuma bintiye Mtume Muhammad zinaenea kote kote na kwamba kila nchi ilipashwa sifa hizo hadi Dili na Ulaya. Habari zinaenea kwa waasi na makafiri walio Sitambuli na Kistantania.

Sifa za uzuri wa Fatuma zinaenea na kuwa kila mmoja anashangaa na kuduwaa, hali inayowafanya watu wakose la kunena kwa ajili ya sifa zinazoenea dunia nzima. Wafalme wote

katika mawazo yao wanatafakari na kujisemeza kuwa watajiamini kumposa Fatuma kwa ajili ya sifa nzuri za urembo alizonazo. Kwa hivyo posa zinatumwa nyingi kutoka kwa wachumba wengi wakiwemo Waislamu na makafiri kwa nia ya kumwoa Fatuma bintiye Mtume Muhammad. Kila mmoja anaharakisha kupeleka barua ya posa huku akijisemea moyoni kuwa ni yeye tu ndiye atakubaliwa kumwoa Fatuma.

La ajabu ni kuwa kila anayemposa Fatuma, binti ya Mtume Muhammad, iwe kupitia kwa waraka au kwa kumtuma mjumbe, Mtume hakuupokea ujumbe wala kukubaliana nao, bali Mtume aliwajibu kwa maneno yake mwenyewe. Mtume anakataa mambo yao kwa kuwapatia jibu ambalo si baya au nzuri, kwani anaendelea kuingojea ishara kutoka kwa Mungu ikishushwa kwake. Mtume ana imani kubwa kuwa ni Mungu pekee ndiye aliye na uwezo wa kupeana mchumba. Mtume anaingojea amri kutoka kwa Mungu ndiposa aifuate.

Watu wasi Waislamu wanaamua kuslimu na familia zao zote ili wawe waislamu kwa ajili ya kutaka kumposa Fatuma. Hata hivyo wanapopeleka posa Mtume hakuridhika na posa zao bali aliwaptia jibu lake la kutompatia mtu matumaini au kuwakataa. Hali ya kutompatia mtu matumaini ya kumwoa Fatuma ilikuwa njia moja ya kuwapatia nafasi waliomposa Fatuma kutafuta wengine wa kuwaposa na kuwa kuliko kupoteza wakati wakitarajia kumwoa Fatuma. Kila wakati Mtume alimwambia Mungu kuwa yeye hakuwa na watoto wala harusi kwani ni Mungu pekee yake anayeiwezesha harusi ifanyike. Mtume alijua kuwa uamuzi juu ya Fatuma ulikuwa mikononi mwa Mungu ambaye ni karimu na kuwa hakuna anayeweza kuipinga amri yake. Kwa sababu ya uelewa huo, Mtume Muhammad anatarajia kutoka kwa Mungu na anaapa kuwa kile Mungu anampatia atakichukua kwa furaha.

Kwa kuwa watoto wa kike hushauriwa na mama na mamake Fatuma amekufa basi tunaona kuwa Fatuma anakosa wa kumshauri.  Mtume Muhammad anamwona Mungu kama

mshauri na kuwa kutakapotokea wa kumposa Fatuma ni Mungu pekee ndiye atakayeweza kuamua mume anayemfaa hasa kati ya watwana wake. Mtume Muhammad anamwomba Mungu kuwa ampatie Fatuma mume mzuri na karimu na kuwa yeye baba ya Fatuma hawezi kumchagulia kwani hajui mume anayemfaa binti yake. Baada ya maombi mtume ananyamaza anamsifu, anamshukuru Mungu na kuungojea mradi wa Mungu kwa kuwa Mungu pekee ndiye mwenyezi.

**2.6 Uhusiano kati ya Ali na Muhammad.**

Ali Talibu anasilimu akiwa bado mvulana mdogo na kuwa mwaminifu baada ya kifo cha baba yake. Mtume Muhammad anamchukua Ali baada ya kuishi naye kwa sababu ni ami wa Mtume Muhammad. Kwa hivyo uhusiano ulioko unampatia Ali kibali cha kurithi kutoka kwa Mtume. Ali anampenda Fatuma lakini kwa sababu ya ufukara alio nao inakuwa vigumu kumposa Fatuma. Ali anaamua kumwomba Mungu kwa ajili ya ndoa. Mungu anamjibu kwa kumpatia Fatuma kama mke wake siku ya Ijumaa.

**2.7 Allah anaamuru matayarisho ya harusi.**

Allah anamwamuru Malaika Jibrili kuwaita malaika wengi wasihesabika ili wawe mashahidi. Malaika Jibrili anapaza sauti na kuwaita na kukutanika enzini kuupokea ujumbe. Malaika wanatulia na kungojea kupashwa ujumbe. Mungu anamwita Malailka Jibrili na kumpa ujumbe na kumwamuru kuenda kwa haraka Peponi kumwamuru Ridhiwani kuipamba. Kila pahali palistahili kupambwa na kuwa kila aliyepatikana Peponi alistahili kuwa amejipamba kwa ajili ya harusi kati ya Ali na Fatuma. Malango yote ya Peponi yalistahili kufunguliwa wazi na yale ya kuzimuni yalistahili kufungwa kiasi kwamba hapangekuwa na mwanya wa mtu, barabara

pia zilistahili kupambwa kwa ajili ya harusi kati ya Ali na Fatuma. Baada ya Ridhiwani kuipamba Peponi, Malaika Jibrili alitumwa na Mungu kwenda Peponi kufukiza matukio ya sampuli tofautitofauti.

**2.8 Ufafanuzi juu ya harusi**

Malaika walikuwa wakishughulika na matayarisho na maandalizi ya harusi bila kujua maharusi ni akina nani. Kwa hivyo baada ya shughuli ya maandalizi na matayarisho ya Peponi kumalizika, malaika walitaka kujua maharusi. Malaika walimwuliza Malaika Jibrili kwa sababu wao walijua kuwa harusi haikumhusu yeyote kati yao. Mungu katika ukuu wake aliwaeleza kuwa hiyo ilikuwa siku ya harusi na kuwa anamwoa msichana bikira, mwanamke bora zaidi kati ya wanawake wengi ambaye ni Fatuma bintiye Mtume Muhammad, Mungu anamwoza kwa Ali ambaye ni mwombezi. Mungu aliwafafanulia na kuwaondolea wasiwasi na sitofahamu ambayo walikuwa nayo kwa ajili ya maandalizi na matayarisho waliyokuwa wameyafanya.

**2.9 Ndoa takatifu mbinguni na duniani.**

Baada ya maandalizi na matayarisho Mungu aliandaa vyakula na kuwaalika wageni kushuhudia ndoa kati ya Ali na Fatuma mbinguni. Hapo Malaika Jibrili anamwakilisha Ali, Mungu akawa hakimu wa Fatuma, Malaika Mikaili akawaunganisha maharusi nao malaika wanne wakawa mashahidi. Harusi ilipokamilika mbinguni, Mungu aliwatuma malaika 70,000 wakiongozwa na Malaika Jibrili wapeleke ujumbe duniani. Mungu aliwapatia mahari ya kumpelekea Mtume Muhammad kwa niaba ya Ali kwa ajili ya kumwoa Fatuma. Mahari waliyompelekea Mtume yalikuwa ya thamani isiyopatikana duniani. Mtume Muhammad Alipokea ujumbe kwa furaha na kwenda kumpasha bintiye. Fatuma alipopashwa habari hiyo

anakubali kuolewa kwa Ali lakini anakataa mahari. Fatuma alimtuma baba yake awaarifu malaika kuwa angependa apewe na Mungu kibali cha kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake Waislamu siku ya kiama. Malaika Jibrili anamrudishia Mungu ujumbe wa Fatuma, Mungu anamtuma na aya kumpelekea Fatuma. Fatuma anaifunga aya kwa uzi na kuivalia kama hirizi kwenye shingo lake.

Jioni ilipofika Mtume Muhammad alimwandaa binti yake na kumpeleka kwa Ali wakiandamana na malaika na wanawake wa tabaka la juu. Ali alimpokea Fatuma kwa furaha nyumbani kwake na walioandamana na Fatuma wakarudi makwao na kuwaacha maarusi pekee yao. Siku iliyofuata asubuhi Ali na Fatuma walipoamka walikuwa wanahisi njaa, katika nyumba ya Ali hamkuwa na chochote cha kula. Ali anaamua kwenda kutafuta kazi ili apate pesa za kununulia chakula. Alienda Shamu bila kumwarifu yeyote ambako alipata kazi na kulipwa mshahara wa peni tatu.

**2.10 Safari ya kutoka Shamu kurudi Madina.**

Ali alipolipwa mshahara aliamua kurudi nyumbanin na akiwa njiani anakutana na maskini watatu ambao aliwapatia hizo peni tatu na kubaki bila chochote. Akiwa njiani huku ametekwa na mawazo kwa sababu pesa alizotarajia kununulia chakula amewasaidia zote, mbele yake kunatokezea ghafla kijana na ngamia. Kijana alimtaka Ali anunue ngamia lakini Ali hakuwa na pesa za kumnunua. Kijana huyo alikubali kumuuzia Ali ngamia kwa deni. Baada ya Ali kuachana na kijana aliyekuwa na ngamia, Ali alikutana na Mwarabu ambaye alikuwa tayari kumnunua ngamia. Mwarabu alimpokeza Ali mfuko uliojaa dinari kwa ajili ya malipo ya ngamia.

Baada ya Ali kupewa hizo dinari alienda moja kwa moja hadi kwa Mtume Muhammad. Mtume alipomwona hata kabla Ali amwelezee chochote kuhusu safari yake ya kutoka Shamu, Mtume alimweleza kana kwamba yeye Mtume ndiye aliyeshuhudia. Mtume alimfafanulia kwa undani aliokutana nao alipokuwa njiani kutoka Shamu akiwa anarudi Madina. Baada ya Mtume Muhammad kumweleza na kumfafanulia Ali yote aliyoyashuhudia, Ali alienda nyumbani kwa mke wake. Alipofika kwa mke wake alimweleza yote aliyoyashuhudia, wote wakafurahi kwa ajili ya uwezo wa Mungu, Kwa sababu walikuwa na pesa nyingi, waliandaa karamu kubwa ya harusi na kuwaalika wageni. Baada ya harusi, pesa walizosalia nazo walizitoa kama sadaka. Katika ndoa yao Mungu aliwabariki na watoto wawili wavulana ambao walikuwa Hasani na Huseini.

### 2.11 Wasia wa Fatuma

Kwa vile Fatuma alimwomba Mungu kuwa alitamani kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake wa Kiislamu, Mungu alimteremshia aya kutoka mbinguni kupitia kwa Malaika Jibrili na kushonelea uzi na kuivalia kama hirizi shingoni mwake. Aliamua kumweleza Ali kuwa angependa wakati atakufa asitolewe hirizi iliyo shingoni mwake. Hirizi aliyokuwa amevalia Fatuma ilistahili kuwa kitambulisho mbele ya Mungu kuwa yeye ni mtetezi na mwombezi wa wanawake, Fatuma angeivua hiyo hirizi atakapofika mbele ya Mungu.

### 2.12 Matukio ya kiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*

Matukio ya kiajabu ni matukio ambayo si ya kawaida iwapo tutayaweka katika ulimwengu wa kawaida. Haya ni matukio ambayo ni kinyume na matukio ya kawaida yanavyotarajiwa na binadamu wa kawaida. Mtunzi wa utenzi huu, katika utunzi wake,

ameyasawiri matukio ya kiajabu kama kwamba ni ya kawaida, lakini kwa mtu wa kawaida anayeusoma utenzi wenyewe anayaona si ya kawaida jinsi mtunzi anayachukulia. Matukio yenyewe ni kama yafuatayo: - harusi kufanyika mbinguni, malaika kuteremsha mahari kutoka mbinguni hadi duniani na Ali kukutana na muuza ngamia na mnunuzi wa ngamia anayemlipa pesa nyingi.

**2.13 Uzuri wa Fatuma**

Mtunzi ameutukuza urembo wa Fatuma kiasi kuwa yeyote anayezisoma sifa za urembo huu anashangaa kama Fatuma ni binadamu au ni malaika. Mtunzi anadai kuwa kadri Fatuma anavyoendelea kukua ndivyo urembo wake unavyokua zaidi. Inasemekana kuwa uso wa Fatuma una nuru ambayo ni zaidi ya mwezi na kuwa mwanadamu yeyote anayemtazama anaridhika. Mtunzi anadai kuwa hakuna bikira anayelinganishwa na Fatuma kwani Binti yake Mtume halinganishwi. Rangi ya ngozi ya mwili wake na tabia zake hakuna anayemfikia. Kwa hivyo sifa nyingi juu ya uzuri wa Fatuma anazomiminiwa zinawapelekea wasomi wa utenzi huu kuchukuliwa kuwa ni tukio la kiajabu. Mtu wa kawaida huwa na uzuri kiasi na si kupita kiasi mpaka dunia nzima ijue (ub. 91-96).

Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* mtunzi anaeleza juu ya sifa za uzuri wa Fatuma binti yake Mtume Muhammad zinavyoenea Uarabuni, Yamani, Uswisi, Damaski, Basara, Iraki, Dili, Ulaya, na sehemu zote za dunia. Inakuwa vigumu sana kuelewa jinsi ambavyo ujumbe juu ya sifa za Fatuma ulivyoenea na muda ambao huo ujumbe ulichukua kuenea pembe zote za dunia. Vilevile unashangaa kwa nini uzuri wa msichana mmoja tu utawaathiri watu duniani kote na kuwa urembo huo ujulikane na karibu kila mtu duniani. Anayesoma huu utenzi huu atashangaa iwapo Fatuma ni mwanamke wa hapa duniani au ni malaika wa mbinguni (ub. 111-124).

## 2.14 Uhusiano wa Mtume Muhammad na Binti yake Fatuma

Uhusiano uliokuwepo kati ya Mtume Muhammad na Fatuma binti yake ulikuwa wa ajabu kwani mtunzi anasema kuwa Mtume kwa ajili ya upendo mwingi kwa mwanawe hangemwacha kwa vyovyote popote alipokuwa. Kila wakati Mtume anapoenda kusali Msikitini na kurudi nyumbani Fatuma alikuwa anamlaki na kuwa anapotaka kutoka aelekee popote alimwita Fatuma kwa jina "nyota" naye aliruka juu na kumkimbilia. Vilevile inasemekana kuwa kila wakati Mtume Muhammad alipomwona Fatuma alimwomba Mungu kumsamehe. Matukio haya si ya kawaida hata kidogo, ni kweli baba anastahili kumpenda mwanawe lakini unapouona upendo kati ya Mtume Muhammad na bintiye Fatuma ni upendo ambao ni wa kupita kiasi. Vile vile tunavyoelewa kuwa unafika umri hasa wa kuvunja ungo ambapo mtoto wa kike hatakuwa huru sana na baba yake lakini uhusiano kati ya Mtume na Fatuma mpaka haupo hata kidogo. Tunapata kuwa kila wakati Mtume Muhammad anataka awe karibu na Fatuma, Fatuma anaruka kwa kumkimbilia baba yake. Haya hata kama yanatendeka sisi tunaosoma, tunayaona kuwa si matukio ya kawaida. Mfano katika Utenzi:-

Endapo alikimwita: "nilia, ewe nyota"

Fatuma akayivuta, mbeleze akimwemea (ub. 99).

Mtunzi anatuelezea kuwa Fatuma anapovunja ungo anaendelea kuzidi katika wema na nuru ilimzangaa. Hali hii ya Fatuma inamweka Mtume Muhammad katika wasi wasi kila wakati. Mtume anatamani sana kumjua atakayemwoa Fatuma. Hili ni tukio la kiajabu kwa sababu uzuri wa mtoto msichana hauwezi kumtia wasiwasi baba mzazi mpaka atamani sana kutaka kumjua atakayemwoa msichana wake. Kwa kawaida urembo wa mtoto wa kike huwa ni furaha kwa wazazi na si tena jambo la kuwazia na kumsumbua mzazi (ub. 108-110).

Unapofika wakati wa Fatuma kuozwa kwa Ali, Mtume Muhammad ndiye anayemwandaa binti yake. Mtume Muhammad anamfunika binti yake kwa mavazi maridadi, anampaka mafuta ya manukato na kumfukizia marashi ya bei ghali. Shughuli hii Mtume Muhammad anaifanya akiwa pekee yake, jambo ambalo si la kawaida kwa sababu shughuli ya kumpamba na kumtayarisha bibi arusi hufanywa na akina mama na wala si jukumu la mwanamume. Hata kama mama yake Fatuma alikuwa ameaga, Mtume angewahusisha wanawake waliokuwa karibu naye. Kwa sababu wakati anapompeleka Fatuma kwa Ali inasemekana kuwa wanawake wa tabaka la juu wanaandamana na Mtume. Jambo hili lina maana kuwa kulikuwa na wanawake ambao wangejishughulisha katika kumtayarisha na kumpamba bibi harusi ambaye ni Fatuma (ub. 317-320).

**2.15 Posa ya Fatuma**

Posa ya Fatuma ni tukio la kiajabu kwa sababu mtunzi anadai kuwa kila aliyezisikia sifa za urembo wa Fatuma alituma posa kwa Mtume Muhammad. Watu wengi wa tabaka tofauti tofauti walituma posa ili wakubaliwe kumwoa Fatuma. Waliotuma posa zao ni pamoja na masultani, Waislamu, makafiri na hata wengine wasi Waislamu waliamua kuslimu na familia zao zote kwa ajili ya kutaka kumwoa Fatuma. Hawa wote walituma wajumbe kupeleka posa na wengine walijipeleka wenyewe, kila mmoja akiwa na matarajio ya kumwoa Fatuma. Hili ni tukio la kiajabu kwa sababu si jambo la kawaida kila mmoja anayesikia sifa za uzuri wa mshichana atataka kumposa. Si kawaida kila mwanamume kutaka kumposa mshichana ili aweze kumwoa hata bila kumwona na kumwelewa (ub. 111-124).

Jibu ambalo Mtume Muhammad anawapatia wanaomposa binti yake ni jibu ambalo si baya au zuri ni tukio la kiajabu. Mara nyingi majibu ya posa huwa baya au zuri na kwa hivyo

wakati mwingi jibu kama hilo husababisha uhusiano mzuri au uhasama kati ya familia husika. Lakini kulingana na Mtume Muhammad aliamua kutopeana jibu ambalo lingeathiri uhusiano wake na wahusika yaani waliomposa binti yake na familia zao uendelee kuwa bora hata kama hawajapata nafasi ya kumwoa.

**2.16 Matayarisho ya ndoa ya Fatuma**

Kuna matukio ya kiajabu katika maandalizi na shughuli za harusi ya Fatuma. Katika utenzi huu matayarisho ya harushi ya Fatuma yanafanyika mbinguni ambapo malaika anaamrishwa na Mungu kuwaita malaika wenzake na kuwagawanyia kazi watakazozifanya katika maandalizi ya harusi ya Fatuma. Inasemekana kuwa Peponi kunaandaliwa na kupambwa sawasawa na malango ya kuzimuni yanafungwa huku manukato yakifukizwa. Maandalizi haya na matayarisho hayo yanavyoelezwa ni kana kwamba yanafanyika hapa duniani.

Harusi nyingi hufanyika duniani pekee na wala si mbinguni. Tunakubali kuwa harusi hufanywa mbinguni lakini hata kama hufanyika si jinsi harusi ya Fatuma inavyofanyika kwani harusi yake inahusisha matayarisho ambayo yanafanywa na malaika wanaoamriwa na Mungu. Kwa hivyo harusi ya Fatuma mbinguni ni tukio la kiajabu (ub. 133-183).

Vilevile wakati wa harusi yenyewe inafanyika mbinguni ambapo malaika Jibrili anamwakilisha Ali, Mungu anakua hakimu wa Fatuma, malaika Mikaili anawaunganisha maharusi nao malaika wanne wanawakilisha kama mashahidi. Tukio hili ni la kiajabu kwani kuunganishwa kwa maharusi kunafanyika mbinguni na ilhali wahusika hawajui kuwa shughuli kama hiyo inafanyika kwa kawaida ndiposa harusi ifanyike lazima maharusi wajue na wahusike (ub. 230-239).

Kwa kawaida mume anayenuia kuoa mke ndiye anayestahili kumlipa mke wake mahari, kwa hivyo Ali anastahili kumlipa Fatuma mahari lakini hana chochote cha kulipa mahari. Kwa hivyo badala ya Ali kumlipa Fatuma mahari, Mungu ndiye anateremsha mahari kutoka mbinguni na anawatuma malaika ambao wanampelekea Mtume Muhammad kwa niaba ya Ali. Mungu kuwatuma malaika na mahari kushushwa kutoka mbinguni ni tukio ambalo si la kawaida. Kwa kuwa malaika walishuka kutoka mbinguni wakiwa wamebeba mafungu na vifurushi vya mali ya thamani kama fedha, dhahabu, johari na mavazi ya bei ghali kutoka Peponi (ub. 240-261).

Tukio jingine la kiajabu ni pale ambapo Fatuma anapelekewa mahari kisha anakataa. Malaika wanapoleta mahari kutoka mbinguni wakiongozwa na malaika Jibrili, Fatuma anakubali ndoa kati yake na Ali lakini anakataa mahari ambayo ni mali ya thamani. Hali ya Fatuma kukataa mahari ni tukio la kiajabu kwani katika hali ya kawaida kwa msichana wakawaida angekimbilia kuichukua mali hiyo kwa ajili ya thamani yake. Vilevile Fatuma ni mwanamke wa ajabu kwa sababu anaamua kupinga mahari kutoka kwa Mungu, anakua na ujasiri wa kumwambia baba yake amwambie Malaika Jibrili amwambie Mungu kuwa hataki mahari. Kwa kawaida binadamu wa kawaida ana imani kuwa chochote Mungu amepatiana kinastahili kukubalika bila swali. Kwake Fatuma ni tofauti kwani yeye anakataa mahari na inarudishwa mbinguni kwa Mungu kinyume na matarajio ya binadamu wa kawaida (ub. 293-295).

Wakati wa maandalizi ya harusi ya Fatuma kule mbinguni inasemekana kuwa kila mahali panapambwa na hata ghorofa zote nane zinapabwa. Hii ina maana kuwa hizo ghorofa zote zilitarajiwa kujaa na watu kwa hivyo anayetafakari juu wingi wa watu waliohudhuria sherehe ya Ali na Fatuma. Hii hali inaashiria wingi wa watu usi wa kawaida kwa sababu peponi yote ilitakiwa kujaa kwa ajili ya sherehe ya harusi.

Wakati wa matayarisho ya kuipamba peponi malaika wanafikia wakati ambapo wanataka kujua ukweli na sababu ya matayarisho hayo, kwa hivyo wanamuuliza Mungu awafafanulie. Mungu anawambia kuwa ni harusi inayotarajiwa. Malaika wanamwambia Mungu kuwa hakuwapatia hisia za mapenzi na kuwa wao si wanaume wala wanawake. Hapa inakuwa ni vigumu kuelewa iwapo mbinguni hakuna wanaume wala wanawake majina kama malaika, Jibrili, Mikaili ni ya jinsia gani? Ama yanatumika na yeyote aliye mbinguni mradi awe malaika.

"hakututia moyoni, shahawa ya kutamani"

Hatukuwa nisiwani, walau hutu rijaa (ub. 223).

Katika ubeti, huu inajitokezea kuwa mbinguni hakuna chochote kuhusiana na jinsia, lakini tena kwenye (ub. 178) tunaelezwa kuwa hata wavulana na watoto wa peponi wanastahili kupambwa kwa ajili ya harusi ya Ali na Fatuma. Tunavyojua mvulana ni jinsia ya kiume na kuwa ndipo tuwe na watoto lazima kuwe na jinsia ya kike wanaowazaa. Tukio la kiajabu linatokezea pale inakuwa vigumu kuelewa kama ni kweli mbinguni hakuna chochote kuhusiana na jinsia, ama kama kuna swala la jinsia na kama halipo hawa wavulana na watoto wanatokezea wapi? Ubeti wenyewe ni:

Hata nao ghilmani, pamoya na wildani

Na waipambe yakini, mapambo yaso misaa! (ub. 178).

Tukio jingine la kiajabu linadhihirika wakati wa harusi ya Ali na Fatuma, pale Mungu anaamuru malango ya peponi yafunguliwe zaidi kiasi kwamba mtu yeyote anayeyaona yalivyofunguliwa ashangae. Amri inatolewa kuwa malango ya kuzimuni yote yafungwe kiasi kwamba hata hakubakii na mwanya wa mtu kuchungulia. Haya yote yanafanywa kwa ajili ya kumshangaza na kumfungia mtu ambaye anachukuliwa kuwa wa kawaida. Kwa kawaida mbinguni viumbe wanaopatikana huko ni malaika na wala si watu wa kawaida. Jambo hili

linamfanya msomi wa utenzi huu kujiuliza kama mbinguni bali na malaika wanaoishi huko, pia watu wakawaida wanapatikana huko.

Malango yote ya peponi kufunguliwa hakuna uhusiano wowote hata kidogo katika harusi za duniani. Tunavyoelewa ni kuwa shughuli ya harusi inafanyika bila hao maharusi kuwepo kule mbinguni kwani wao wako duniani. Harusi ya Ali na Fatuma ni ya kweli si ya kifikirika tu bali inafanyika mbinguni na wageni wanaohudhuria harusi hiyo wanaishuhudia. Kwa kawaida harusi nyingi hufanyika duniani tu na iwapo kunakuwa na nyingine mbinguni basi ni kwa kufikiria na wala si halisi. Kwa kawaida harusi huwa moja tu lakini kwao Ali na Fatuma ni mbili ambapo moja inafanyika mbinguni na ya pili duniani (ub. 230-239).

Kuhusika kwa Mungu na malaika katika maandalizi na shughuli ya harusi kati ya Ali na Fatuma ni tukio ambalo si la kawaida. Hapa Mungu na malaika wanahusika kikamilifu si eti miujiza ndiyo inayooneka au kutendeka tu, bali Mungu binafsi anahusika Mungu ndiye anayetoa amri kwa malaika Jibrili ambaye anawaamuru malaika kama Radhiiwani kuipamba peponi kwa ajili ya harusi kati ya Ali na Fatuma. Unapowadia wakati wa siku ya harusi kunakuwa na kugawana majukumu kati ya Mungu na malaika ambapo Mungu ni hakimu wa Fatuma bintiye Mtume Muhammad, malaika Jibrili ambaye anawaamuru malaika kama Ridhiwani kuipamba peponi kwa ajili ya harusi ya Ali na Fatuma.

Unapowadia wakati wa siku ya harusi kunakuwa na kugawana majukumu kati ya Mungu na malaika ambapo Mungu ni hakimu wa Fatuma bintiye Mtume Muhammad, malaika Jibrili anamwakilisha Ali, malaika wanne wanakuwa mashahidi naye malaika Mikaili anahalalisha ndoa kwa kuwaunganisha Ali na Fatuma. Kwa hivyo tunakubaliana kuwa Mungu na malaika wanahusika katika ndoa ya Ali na Fatuma kikamilifu kule mbinguni. Vilevile Mungu anawatuma malaika duniani kumpelekea Mtume Muhammad mahari kwa ajili ya harusi ya Fatuma. Malaika

wanabeba mali kulingana na uwezo wao kupeleka duniani. Kwa ajili ya uwezo mkuu wa Mungu, angeshusha mahari moja kwa moja kutoka mbinguni lakini anaamua kuwahusisha malaika (ub. 240-261).

**2.17 Maisha ya Ali**

Umaskini unaotajwa kumhusu Ali ni umaskini usi wa kawaida kwani hakuwa na chochote. Ufukara alio nao Ali unamzuia kumposa Fatuma hata ingawa anazo hisia za mapenzi kwa Fatuma. Kwa kawaida kuna watu fukara lakini ufukara alio nao Ali ni ufukara kupita kiasi mpaka inasemekana kuwa hana hata mbegu moja. Ali kwa ajili ya ufukara anaficha hisia zake za mapenzi. Hili si jambo la kawaida kwani mara kwa mara kumekuwepo na hali ambapo mtu kutoka familia ya tabaka la chini zaidi anamwoa mke kutoka tabaka la juu na wanaishi. Tujuavyo penzi halifichiki kwa hivyo ufukara hauwezi kuwa sababu kuu ya kutopenda. (ub. 145-149).

Baada ya Fatuma kupelekwa kwa Ali na baba yake ambaye ni Mtume Muhammad, maharusi hawa wanalala lakini kunapopambaza asubuhi wanahisi njaa na wanahitaji kula. Jambo la ajabu ni kuwa ndani ya nyumba ya Ali hamukuwa na chochote cha kula. Inadaiwa kuwa Ali anajaribu kusakanya kila mahali lakini hapati chakula ambacho anaweza kumpatia mke wake ale. Tunavyoelewa ni kuwa mume anapotarajia kuoa hufanya juu chini kuwa na kile anawezakutumia baada ya kuoa. Hali aliyo nayo Ali ni ya ajabu kwa sababu hata baada ya kufanyiwa kila kitu kuhusiana na harusi bado hana chakula cha kumwandalia mke wake. Kusakanya kila mahali lakini hapati chakula ambacho anaqweza kumpatia mke wake ale. Ali anasakanya kila mahali ndani ya nyumba bila kupata hata mbegu moja hali inayomfanya apatwe na aibu mbele ya mke wake. Vilevile ni tukio la ajabu pale ambapo Ali anatafuta kile anajua vizuri kuwa hakipo, anatafuta chakula ndani ya nyumba na kila mahali na anajua tosha kuwa

hajakinunua chakula anachokitafuta. Mara kwa mara mtu hutafuta kile anajua kuwa kipo na katika hali ya kusahau ndiposa ataamua kukitafuta alipokiweka (ub. 330-335).

Safari ya Ali kutoka Madina kurudi Shamu ni tukio la kiajabu pale tunamwona Ali anakutana na maskini watatu ambao wanamwomba pesa na anaamua kuwapatia peni tatu zote na kusalia bila chochote. Hili ni tukio la kiajabu kwa sababu kwa kawaida mtu si rahisi asaidiane pesa zake ambazo ametolea jasho mpaka ziishe atajaribu awezavsyo angalau kujibakishia kiasi. Lakini kwake Ali anaamua kuwasaidia maskini pesa zake zote na kusahau kuwa sababu ya kwenda kutafuta kazi ilikuwa ni njaa waliyokuwa nayo yeye na mkewe. Ali anasaidiana pesa zote mpaka baada ya kutoa peni la mwisho anajihisi ni kama hana hata nguvu za kumwezesha kutembea. Hali ya Ali kuishahau nja aliyo nayo na kuhusika katika hali ya umaskini wa wengine ni jambo la ajabu (ub. 345-364).

Baada ya Ali kuwasaidia maskini na hela zake zote anakutana na kijana ambaye ana ngamia, wanaongea kidogo  na kijana huyo anaamua kumuuzia ngamia kwa deni na bei rahisi. Ali hakumjua kijana huyo lakini wanakubaliana kuwa atamlipa baadaye. Ali anaendelea na safari yake na kisha anakutana na Mwarabu ambaye anakubali kumnunulia ngamia ambaye Ali anaye na anampatia mfuko ambao umejaa dinari na kuenda na ngamia. Hawa watu wawili Ali hawajui lakini shughuli ya kununua na kuuza ngamia inafanyika bila shida yoyote. Jambo hili kwa hali halisi ni gumu na haliwezi kufanyika lakini kwake Ali linafaulu.

Baada ya Ali kumuuza ngamia na kupewa pesa nyingi sana anakuwa tajiri asiyetajika. Hali yake ya maisha inabadilika muda mfupi kutoka umaskini hadi utajiri (ub. 365-408). Hali ya Mtume Muhammad kumwelezea Ali yote aliyokumbana nayo alipokuwa anatoka Madina kurudi Shamu ni tukio la kiajabu. Kwa sababu ni Ali mwenyewe aliyekumbana na hali hizo naye Mtume hakuwa wakati huo lakini kabla Ali amwelezee Mtume, Mtume anamweleza kana

kwamba aliyaona yaliyotendeka. Mtume anamweleza juu ya maskini ambao Ali alikutana nao, shughuli ya kuuza na kununua ngamia na anamfafanulia juu ya wote ambao alikutana nao. Maelezo ya Mtume Muhammad yanamshangaza Ali. Hili ni tukio la kiajabu kwa sababu Mtume anaeleza mambo ambayo kwa kweli si yeye aliyekumbana nayo (ub. 389-405).

Ali kwenda kwa Mtume Muhammad baada ya kumuuza ngamia ni tukio la kiajabu kwa sababu tunatarajia mara tu anapomuuza awe na shauku ya kuenda kwa mpenzi wake Fatuma. Anastahili kwenda kwa Fatuma ili wafurahie baraka ambazo amepata kama mume na mke lakini yeye anaamua kwenda kwa babamkwe. Vilevile tunavyojua ni kuwa ni kwa sababu ya njaa ambayo walikua nayo kama mume na mke ndiyo ilimpeleka kwenda kutafuta kazi ili apate pesa za kununulia chakula na tunamwona ni kama amesahau njaa aliyomwacha nayo mke wake na kwenda kwa babamkwe kupiga ngumzo (ub. 389-408) .

Ali na Fatuma baada ya kupata pesa nyingi na kuwa wakwasi watajika wanaandaa karamu kubwa ya harusi na kisha pesa wanazosalia nazo wanaamua kutoa sadaka. Wao walifurahia maisha ya ufukara na kwa hivyo baada ya kuzipeana pesa hizo kama sadaka wanayarudia maisha yao ya zamani ambayo ni ya ufukara kwa kawaida Ali na Fatuma wangeamua kujenga nyumba nzuri, wanunue gari, shamba na kuzifanyia shughuli zao za kujinufaisha wenyewe. Hali ya Ali na Fatuma kuamua kuzipeleka pesa zote zilizosalia Msikitini na kuirudia hali yao ya awali ya ufukara ni tukio la kiajabu na wala si la kawaida (ub. 409-551).

## 2.18 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangalia muhtasari wa *Utenzi wa Mwana Fatuma* ambapo tumeangazia utangulizi yaani fomula anayoitumia mtunzi katika kuandika utenzi wake. Tumegundua kuwa mtunzi ameanza kwa kuviomba vifaa vya kutumia katika uandishi wake.

Baada ya mtunzi kuviomba vifaa husika anafuatisha maombi ambapo anamshukuru na kumsifu Mungu kwa makuu yake, Anamshukuru kwa kumuumba Mtume Muhammad, uwezo wa kuumba na kuumbua. Anamsifu Mtume Muhammad kwa sababu alikuwa wa kwanza kuumbwa kabla ya mitume wengine wote. Nuru ya Mtume iliumbwa na ikanawiri sana yeye ndiye mwenye baraka aliyepanda mbingu saba. Malaika huomba kupitia kwake na kuwa Mungu anaamuru Mtume Muhammad aombewe mchana na usiku.

Tumeliangazia lengo la utenzi, vilivyo bora vinne lakini kimoja ni bora zaidi kuliko vingine kati yavyo ni malaika, Iziraili anayetenda kazi nyingi kwa ajili ya kumtoa mtu uhai, kati ya vitabu vitakatifu Mungu alichagua Kurani Takitifu, kati ya mitume aliye bora zaidi ni Mtume Muhammad, mshirika wa Mtume Muhammad aliye bora zaidi ni Ali mkwe wa Mtume aliyemwua simba na kifaru, mlima ulio bora zaidi ni ule wa Arafia unaojulikana sana, mwezi bora zaidi ni wa Ramadhani.

Tumeziangalia sifa za uzuri wa Fatuma, upendo wa Mtume Muhammad kwa binti yake, kifo cha Khadija mke na kipenzi cha Mtume Muhammad, madhara ya kifo hicho kwani Mtume hakuwa na wakumsaidia katika majukumu ya kulea. Ilimbidi afanye kazi ya Mungu na ahakikishe binti yake ametunzwa vizuri. Binti yake alivyoendelea kukua ndivyo Mtume aliendelea kuwa na wasiwasi juu ya atakayemwoa binti yake. Kuenea kwa posa ya Fatuma mrembo ambapo kila pembe ya dunia imepata kujua juu ya Fatuma kwa ajisli ya urembo wake na kuwa kila mwanamume anayesikia juu ya sifa za urembo wa Fatuma anatamani kumwoa. Posa zinazomfikia Mtume Muhammad kutoka kwa wachumba wengi nchi mbalimbali lakini Mtume hapeani jibu baya au nzuri. Anaamua kumwomba Mungu juu ya swala la ndoa ya binti yake kwani Mtume anajua kuwa Mungu ndiye mwenye uwezo wote.

Maswala mengine ni pamoja na ufukara wa Ali unaomfanya ashindwe kumposa Fatuma na kuamua kumwomba Mungu, jibu linatoka kwa Mungu, maandalizi ya harusi yake Ali , harusi mbinguni, mahari kuletwa kutoka mbinguni kwa Mungu kwa niaba ya Ali, Fatuma kukataa mahari na kusema haja ya moyo wake jambo ambalo Mungu anamtimizia, ndoa ya maharusi hapa duniani. Haja ya Fatuma inatimizwa na Mungu kupitia kwa aya inayoteremshwa na Jibrili hadi kwa Fatuma ambayo anaifunga kwa shingo lake kama hirizi ambayo itamtambulisha mbele ya Mungu kama mtetezi na mwombezi wa wanawake wa Kiislamu. Harusi inafanyika duniani, Ali na Fatuma wanabarikiwa na watoto wa kiume Hassani na Husseini ambao wanawalea kwa upendo. Fatuma anamwambia Ali haja yake kuwa akifa azikwe na hirizi yake shingoni, asitolewe kwani ni ishara ya itakayomtambulisha mbele ya Mungu na hapo ndipo Mungu mwenyewe ataitoa shingoni mwa Fatuma bintiye Mtume Muhammad.

Tumeyachangunua matukio ya kiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* ambapo tumegundua kuwa utenzi huu una matukio mengi ambayo ni ya kiajabu. Matukio yenyewe ni: sifa za urembo wa Fatuma, upendo kati yake na baba yake Mtume Muhammad, ufukara kupindukia alionao Ali. Posa na ndoa ya Fatuma ni matukio ya kiajabu kwani urembo wa kupindukia wake unajulikana kila sehemu na kuenea pembe zote za dunia kwa hivyo kusababisha kila mwanaume kutuma posa ya kutaka kumwoa.

Harusi ya Fatuma inaandaliwa na kufanyika mbinguni ambapo Mungu na malaika wakihusika kikamilifu. Mahari ya Fatuma ni tukio la kiajabu kwani Mungu ndiye anawapatia malaika kumpelekea Mtume Muhammad ambaye anastahili kumpatia Fatuma. Mahari hiyo inatoka mbinguni kwa sababu Ali hana uwezo wa kulipa kwa hivyo analipiwa na Mungu. Matukio mengine ni pamoja na: Ali kuwasaidia maskini na pesa zote anazopata baada ya kufanya kazi mpaka anasalia bila kitu kwa ajili ya maskini watatu. Ali anakutana na asiyemjua

anampatia ngamia kwa deni na baadaye anamuuza pesa nyingi zinazobadilisha maisha yao. Ali na Fatuma wanatoa pesa walizobakia nazo kama sadaka baada ya kuandaa harusi yao duniani na wanarudia hali yao ya umaskini ambayo wanaifurahia. Kwa hivyo tumeangazia muhtasari wa *Utenzi wa Mwana Fatuma* na kuyachaganua matukio ya kiajabu yanavyojitokeza.

# SURA YA TATU

## SIFA ZA KIUHALISIAJABU KATIKA *UTENZI WA MWANA FATUMA.*

### 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tumeangalia muhtasari wa *Utenzi wa Mwana Fatuma* na matukio ya kiajabu ambayo yameibuka. Sura ya tatu tumeshughulikia sifa za kiuhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Sifa za kiuhalisiajabu tutakazozishughulikia ni pamoja na:- kuwepo kwa wahusika ambao si wa kawaida, matukio ya kiajabu, kuvunjwa kwa mipaka ya mahali pa kufanyika vitendo. Sifa nyingine ya kiuhalisiajabu ni kule kuwepo kwa hali za kushangaza na za kuogofya. Katika uhalisiajabu huwepo wakati ambao ni wa kistari na wa kiduara. Katika kizi ya kifasihi huwepo matukio ya kindoto au ya kifantasia. Mara nyingi wakati wa kazi ya uhalisiajabu hausongi. Mpaka kati ya yanayowezekana, mambo halisia na yasiyowezekana unafutwa.

### 3.1 Matukio yaliyo ya kiajabu ambayo ni ya kushangaza na ya kuogofya.

Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* kuna matukio ya kiajabu ambayo yameimbuka kama njia moja ya kuendeleza utenzi huu. Haya matukio ya kiajabu ni kama vile sifa za uzuri wa kupita kiasi ambazo mtunzi amemmiminia Fatuma ambaye ni bintiye Mtume. Fatuma amepewa sifa ambazo yeyote anayeusoma utenzi huu anabaki akishangaa kama kweli Fatuma ni binadamu wa kawaida ama kama ni malaika kutoka mbinguni. Kwa mfano mtunzi anasema kuwa uso wake Fatuma una nuru iliyo na mwanga mkuu kuliko wa mwezi na kuwa yeyote anayemwona anatosheka kabisa (ub. 92). Anadai kuwa ni bikira anayewashinda bikira wengine kwa sifa na uwezo alionao (ub. 96). Hili ni tukio la kiajabu kwa sababu sifa anazopewa Fatuma si za kawaida. Vilevile inasemekana kuwa kwa sababu ya uzuri wa Fatuma kila pembe ya dunia inapata ujumbe huu na kuwa kila mwanamume anayepata ujumbe huu anatamani kumwoa

Fatuma. Kwa hivyo, posa zinatumwa kwa wingi na hata watu ambao si Waisilamu wanaamua kuslimu na kuwa Waisilamu na familia zao ili wampose Fatuma na kutumainia kumwoa (ub. 80-82). Maandalizi ya harusi ya Fatuma mbinguni ni tukio la kiajabu kwa sababu, kwa kawaida harusi huandaliwa na kufanyika duniani. Harusi ya Fatuma inaandaliwa mbinguni pale Mungu anawaamuru malaika kuhakikisha kuwa Peponi kumepambwa kwa ajili ya harusi ya Fatuma, bintiye Mtume Muhammed. Hali ya harusi ya Fatuma kufanyika mbinguni na kule kuhusika kikamilifu kwa Mungu pamoja na malaika ni jambo la kushangaza. Hali ya Mungu, Malaika Jibrili, Mikaili na malaika wanne kuhusika katika sherehe ya harusi mbinguni kwa kuwakilisha Fatuma na Ali ni jambo la kushangaza kwa sababu hata wakati wa sherehe hiyo hawa wawili hawakuwepo, walikuwa duniani na huenda iwe kuwa hawakujua kilichokuwa kikiendelea kule mbinguni. Ali na Fatuma wanaambiwa na Malaika Jibrili kuwa wameunganishwa kuwa mke na mke baada ya harusi kufanyika mbinguni (ub. 220-306).

Malaika kubeba mahari kutoka mbinguni kumpelekea Mtume duniani kwa ajili ya bintiye ni tukio la kiajabu, kwa sababu kwa kawaida mahari hutolewa duniani kutoka mahali hadi pengine. Lakini hali ya mahari kutumanishwa na Mungu kutoka mbinguni hadi duniani ni jambo ambalo si la kawaida na kwa hivyo hali hii inaipelekea *Utenzi wa Mwana Fatuma* kuwa na sifa ya kiuhalisiajabu kwani ni tukio la kipekee (ub. 240-292).

Fatuma kukubali kuolewa kwa Ali na kukataa mahari ni tukio la kiajabu na la kushangaza. Hii ni kwa sababu binadamu wa kawaida hangekataa mahari yaliyotoka mbinguni. Jinsi ilivyo kwenye utenzi ni kuwa mahari hayo yalikuwa ya thamana na kuwa hayakuwa ya kulinganishwa na mahari ya hapa duniani. Kwa hivyo, tunatarajia Fatuma akubali haraka sana badala yake anakataa kuchukua mahari lakini anakubali kuolewa kwa Ali. Fatuma kukataa mahari ambayo Mungu ametuma ni tukio la kiajabu na la kushangaza. Hii ni kwa sababu, kwa

kawaida, binadamu ana imani kuwa kile Mungu amekubariki nacho unakikubali bila swali lolote. Kwa kuwa hakuna wa kukataa uamuzi wa Mungu. Hata hivyo Fatuma anakataa uamuzi wa Mungu na anapeana haja ya moyo wake. Fatuma anasema:-

“Wa ama mahari, hayo haurizi wangu moyo

Mukhubiri rafikio, kamuarifu Jalia!’ (ub. 295).

Mtume Muhammed kumuandaa na kumtayarisha bintiye kwa kumvalisha, kumpodoa na kumfukiza marashi ni tukio la kiajabu na la kushangaza. Hii ni kwa sababu kwa kawaida huwa ni akina mama ambao humshughulikia bibi harusi anapoandaliwa kwenda kwa mume wake. Badala ya akina mama kufanya hivyo, Mtume mwenyewe anachukua jukumu hilo (ub. 317-322).

Hata kukiwa ioni, Mtume Wethu Amini

Mwanawe kamzayini, kwa libasi na hulia”. (ub. 317).

Matukio mengine ya kiajabu na ya kushangaza ni pale Ali baada ya harusi siku inayofuata wanakosa chakula na hata inambidi atafute na kusakanya kila mahali bila kupata hata mbegu moja (ub. 330-335). Anapokosa chakula kabisa anaamua kwenda Shamu kutafuta kazi. Anapata kazi ambayo analipwa peni tatu, na anaamua kuifunga safari ya kurudi nyumbani Medina. Njiani anakutana na maskini watatu ambao anawasaidia peni zote tatu na kusalia bila chochote. Njiani anakutana na kijana asiyemjua na ngamia. Anakubali kimuuzia ngamia huyo kwa deni. Mbele kidogo anakutana na Mwarabu, anayemnunua ngamia kwa pesa nyingi. Pesa wanazosalia nazo wanaamua kupeana kama sadaka na kurudia hali yao ya ufukara wanayoifurahia (ub. 336-409). Hali hizo zote ni za kiajabu, kwa sababu zinashangaza na hata kuogofya.

### 3.2 Kuvunjwa kwa mipaka ya mahali

Matukio katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* hayajitokezi katika muktadha finyu wa jamii moja, nchi au hata bara moja. Hali hii imetokezea ili kuondoa ufinyu wa ujumbe ili usiwe ujumbe wa watu au jamii moja tu bali uwe ambao unaweza kuzinufaisha jamii nyingine nchini au mabara mengi pale inapofaa, bila vikwazo vya kitamaduni vya sehemu moja finyu.

Kuna kuvunjwa kwa mipaka ya kimahali katika utenzi huu kwa vile matukio yaliyomo hayajajikiti katika mandhari mahsusi. Hii ni kwa sababu harusi ya Fatuma inafanyika mbinguni na duniani. Vilevile sifa za uzuri wa Fatuma zinaenea kotekote ulimwenguni na kusababisha idadi kubwa ya wanaotaka kumposa.

Harusi ya Fatuma inafanyika mbinguni baada ya maandalizi yaliyoamriwa na Mungu mwenyewe. Jibrili anapewa amri ambazo anawapelekea malaika wengine kama Ridhiwani ambao wanapaswa kuiunda na kuipamba Peponi inasemekana kuwa inastahili kupambwa ndiposa yeyote atakayeiona atamani kuingia. Wakati Peponi kunapambwa na kufukizwa marashi ya harufu nzuri, malango ya kuzimuni yanafungwa kiasi kwamba hakuna ufa wa kumwezesha mtu kuchungulia (ub. 194 - 200). Baada ya maandalizi, harusi yenyewe inafanyika pale Mungu, Malaika Jibrili na Mikaili wanachukua nafasi zao za kuwakilisha katika harusi hiyo huku kukiwa na malaika wengine wanne ambao ni mashahidi (ub.230-239). Baada ya harusi kufanyika mbinguni harusi ya pili inafanyika duniani ambapo Mungu anawaamuru malaika kupeleka mahari kwa Mtume Muhammad kwa niaba ya Ali (ub. 240-329).

Sifa za uzuri wa Fatuma zinasemekana kuenea kila pembe ya dunia. Yaani kila nchi ilipashwa habari kuhusu sifa za uzuri wa Fatuma. Katika utenzi huu sifa za uzuri wa Fatuma zinaenea Magharibi na Mashariki. Nchi zinazopashwa habari kuhusu uzuri wa Fatuma ni kama Uarabuni, Misri, Uajemi, Uswisi, Damaski, Basara, Iraki, Dili, Uropa na nchi nyingine nyingi

(ub. 112-116). Kwa hivyo kila pembe ya dunia inapata ujumbe huo. Kwa ajili ya kuenea kwa habari hizo ndipo ikawa kuwa kila mwanaume anayepata kuzisikia anatamani sana kumwoa Fatuma. Hali ya kuenea kwa sifa za uzuri wa Fatuma kunapelekea kuwepo kwa posa nyingi kutoka kwa watu tofautitofauti. Posa zinatoka kwa wanaume mbalimbali kutoka nchini mbalimbali duniani. Wanaomposa ni pamoja na masultani, Waisilamu wenzake, makafiri na hata kuna wale wanaoamua kusilimu na familia zao na kuwa Waisilamu wakiwa na matarajio ya kumwoa Fatuma (ub. 116-124).

Mungu anawaamuru malaika, wakiongozwa na Malaika Jibrili, kupeleka mahari duniani kwa niaba ya Ali kwa ajili ya kumwoa Fatuma. Malaika wanabeba mali yenye thamana kupeleka duniani. Baada ya malaika kufika kwa Mtume wanawasilisha ujumbe na mahari. Fatuma anakataa mahari na kwa hivyo Malaika Jibrili anarudi mbinguni kumwelezea Mungu. Mungu anamtuma tena duniani ili Fatuma aseme haja ya moyo wake. Malaika Jibrili anarudi duniani, Fatuma anaulizwa na baba yake haja ya moyo wake. Anajibu kuwa angependa kuwa mtetezi na mwombezi wa wanawake wa Kiislamu.

Malaika Jibrili anarudi mbinguni kumweleza Mungu ambaye anamtuma Jibrili duniani kumpelekea Fatuma aya ambayo anafunga shingoni kama hirizi na ambayo ingemtabulisha mbele ya Mungu kama mwombezi wa wanawake atakapokuwa amekufa (ub. 262-316).

Matukio ambayo tumeyajadili yanaonyesha kuvunjwa kwa mipaka ya mahali kwa sababu matukio haya hayajajikita katika mandhari mahsusi. Kwa mfano, harusi ya Fatuma inafanyika mbinguni na duniani. Mbinguni, Mungu ndiye anawaamuru malaika wakiongozwa na Malaika Jibrili kuandaa na kuipamba Peponi. Malango yote ya Peponi yanafunguliwa wazi kabisa ilhali malango ya kuzimuni yanafungwa kiasi kwamba hakubakii hata mwanya pale mtu anaweza kuchungulia.

Harusi yenyewe inafanyika pale Mungu, Malaika Jibrili, Malaika Mikaili na malaika wengine wanne wanawakilisha katika nafasi zao kila mmoja. Kwa hivyo, mpaka haupo kati ya mbinguni na duniani, kwa sababu shughuli zinazofanyika mbinguni baadaye zinafanyika duniani. Kwa hivyo mpaka wa mahali haupo katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*.

Sifa za uzuri wa Fatuma bintiye Mtume Muhammed zinaenea ulimwengu wote. Sifa hizi hazijabakia kule Fatuma anakozaliwa tu bali zinaenea kila nchi ulimwenguni. Kwa hivyo mpaka wa mahali umevunjwa kwa sababu sifa za uzuri wa Fatuma zinaenea ulimwengu mzima. Kuvunjwa kwa mpaka wa mahali ni pale mahari yanateremshwa kutoka mbinguni hadi duniani. Ndipo mpaka uwepo, inastahili Ali kumpelekea Fatuma mahari hapa duniani na katika nchi yao, lakini Mungu anawatuma malaika na mahari kutoka mbinguni kuleta duniani kwa ajili ya harusi ya Ali na Fatuma.

Posa kwa ajili ya kumwoa Fatuma ni tukio ambalo linajitokeza katika hali ya kuuvunja mpaka wa mahali, kwa sababu baada ya sifa za uzuri wa Fatuma kuenea sehemu zote za ulimwengu, wanaume mbalimbali kutoka nchi mbalimbali wanaamua kutuma posa zao wakitaka wakubaliwe kumwoa Fatuma. Si kwamba ni wanaume wa kijijini pake tu ndio wanamposa, bali wanaume kote ulimwenguni. Hata hivyo wanaomposa Fatuma si wa dini ya Kiislamu pekee yao. Kunao makafiri ambao si Waisilamu wanaomposa. Wengine wasi waislamu wanaamua kusilimu pamoja na familia zao ili wampose Fatuma. Kwa mifano hiyo tunaona kuwa mpaka wa mahali umevunjwa kiasi kwamba mpaka haupo tena.

### 3.3 Matukio yanayozungumziwa ni ya kifantasia

Katika utenzi huu, matukio mengi yanayozungumziwa ni ya kifantasia kwa sababu kuhusiana na sifa za uzuri wa Fatuma inawezekana kuwa sifa alizomiminiwa ziwe za kufikirika

tu. Hii ni kwa sababu jinsi mtunzi anavyozitaja sifa hizo haiwezekani binadamu wa kawaida kuwa na sifa alizo nazo Fatuma. Mtunzi anasema kuwa Fatuma anazidi kuwa na wema na kuwa urembo wake haukukoma. Vilevile uso wake unang'aa zaidi ya mwezi na mwanaume yeyote anayemwona anaridhika (ub. 91-92). Kila kila kitu kwake Fatuma kilikuwa sawa na hakuwa na dosari yoyote hata kati ya bikira wengine waliokuwepo hakuna aliyemshida (ub. 93-96). Haya yote yanajitokeza kama ya kifantasia na si ukweli jinsi mtunzi ameyawasilisha. Mtunzi ametekwa zaidi kimawazo na hayuko katika uhalisi wake.

Sifa za uzuri wa Fatuma kuenea kote ulimwenguni zinavyojitokeza katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* ni tukio la kifantasia. Hii ni kwa sababu sifa za uzuri wa msichana haziwezi kuenea ulimwengu mzima. Kwa hivyo, mtunzi ametekwa na mawazo katika kuwasilisha uzuri wa Fatuma. Inaonekana kuwa kwa ajili ya sifa hizo nzuri, basi ulimwengu mzima utapata habari kumhusu Fatuma. Vilevile mtunzi anadai kuwa posa kwa ajili ya kumwoa Fatuma bintiye Mtume Muhammad zinaletwa kutoka kwa wanaume kote ulimwenguni. Kila mwanaume anayezisikia sifa za uzuri wa Fatuma anajaribu awezavyo kumtuma mjumbe au kujipelekea posa kwa kutaka kumwoa Fatuma.

Wanaume wa tabaka mbalimbali walimposa Fatuma wakiwemo masultani, Waislamu, makafiri na hata wengine kuisilimu pamoja na familia zao kwa nia ya kumposa na kutaka kumwoa Fatuma. Haya yote ni matukio ya kufikirika tu na wala si ukweli halisi kwa sababu hata ukiwa u mrembo kiasi gani si kwamba wanaume ulimwenguni kote watatuma posa kutaka kukuoa. Hali ya ufukara wa Ali unaomfanya asingee juu ya penzi lake kwa Fatuma ni tukio la kifantasia kwa sababu ufukara hauwezi kumzuia mtu kuzieleza hisia zake kwa hivyo mtunzi anapodai kuwa Ali aliona haya kujieleza mbele ya Fatuma na Mtume Muhammad ni la kufikirika tu.

Maandalizi ya sherehe ya harusi ya Ali na Fatuma ni tukio la kifantasia kwa sababu katika hali ya kawaida binadamu hawezi kuyashuhudia matukio yanayotendeka mbinguni. Inaposemekana kuwa Mungu alimwamuru Malaika Jibrili kwenda Peponi kumwamuru Ridhiwani aipambe Peponi ni hali ya kufikiria na wala hakuna ukweli dhabiti. Yawezekana matukio hayo yatendeke mbinguni lakini si kwamba mtunzi aliyashuhudia kwa macho yake. Peponi kunapambwa, kunafukizwa kwa marashi yenye harufu nzuri, malango yote yanafunguliwa wazi na malango ya kuzimuni yanafungwa sawasawa. Harusi kufanyika pale Mungu ni hakimu wa Fatuma, Jibrili anamwakilisha Ali, Mikaili anahalalisha ndoa na malaika wanne wanakuwa mashahidi (ub. 159-239). Matukio haya mtunzi hakuyashuhudia mwenyewe bali alifikiria akilini mwake na kuyatunga.

Mungu anamtuma Malaika Jibrili na wenzake kupeleka mahari kwa Mtume Muhammad duniani kutoka mbinguni. Mahari kutoka mbinguni ni ya thamana kwani mali yenyewe yalikuwa bidhaa za dhahabu, johari, fedha, mawe ya thamani na mavazi ya Peponi. Kila malaika alibeba mali kulingana na uwezo wake. Hili ni jambo la kufikirika kwani mtunzi hakuyashuhudia kwa macho yake mwenyewe. Safari ya malaika kutoka mbinguni kushuka duniani kuleta mahari kwa niaba ya Ali kwa ajili ya kumwoa Fatuma ni jambo la kufikirika. (ub. 240-283).

Safari ambazo Malaika Jibrili anazifanya za duniani na mbinguni ni tukio la kifantasia. Malaika Jibrili anawaongoza wenzake kumpelekea Mtume Muhammad ujumbe wa harusi ya binti yake iliyofanyika mbinguni. Fatuma anakataa mahari, Malaika Jibrili anarudi mbinguni kumwambia Mungu. Mungu anamtuma Jibrili duniani kumuuliza Fatuma haja ya moyo wake. Baada ya Malaika Jibrili kupewa ujumbe na Fatuma, anarudi mbinguni kumpelekea Mungu jibu kutoka kwa Fatuma. Kwa kuwa ni lazima haja ya Fatuma itimizwe Mungu tena anamtuma Malaika

Jibrili kumpelekea Fatuma aya kama ishara ya kukumbalika kwa haja yake ya kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake Waisilamu (ub. 262-316). Safari za mara kwa mara alizozisafari Malaika Jibrili za mbinguni na duniani ni tukio la kifantasia na kuwa hakuna ukweli kuwa mtunzi alishuhudia hali hii.

Harusi kufanyika mbinguni pale Mungu ni hakimu wa Fatuma, malaika Jibrili anamwakilisha Ali, malaika wanne kuwa mashahidi naye Malaika Mikaili kuihalalisha na kuwaunganisha maarusi ni tukio la kifantasia. Hii ni kwa sababu ni baada ya harusi hiyo kufanyika ndipo malaika wanatumwa kwa Mtume Muhammad na ujumbe huo. Hata kwa wakati huo Ali na Fatuma hawakujua kilichokuwa kinaendelea kwani wao hawakuwa mbinguni shughuli ya harusi ilipokuwa inafanyika. Mtunzi amejiingiza katika kufikiria ndipo akayatukia matukio kuhusu harusi mbinguni (ub. 230-239).

### 3.4 Wakati katika kazi za uhalisiajabu hausongi

Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* wakati hausongi kwani matukio yanayojitokeza haieleweki yalichukua muda kiasi gani ndipo yakamilika. Hii ni kwa sababu mtunzi hajaeleza muda ambao hayo matukio yanachukua. Kuenea kwa ujumbe juu ya sifa za urembo wa Fatuma ulimwenguni mzima haujulikani lakini mtunzi katika Utenzi anasema kuwa sifa za urembo wa Fatuma zilienea Magharibi na Mashariki. Haijulikani kama sifa za uzuri wa Fatuma zilichukua siku, miezi au miaka. Vilevile muda ambao posa zilipelekwa kwa Mtume Muhammad kwa ajili ya kumwoa Fatuma haujaelezwa. Mtume Muhammed alingojea kwa muda huku akimwombea binti yake kuhusu ndoa na huku akitamani kumwona mume atakayemwoa Fatuma. Hatuelezwi kiasi cha muda alichongojea ndipo mambo haya yatimike.

Baada ya Ali kuona kuwa ufukara aliokua nao haungemwezesha kumwoa Fatuma, aliamua kumwomba Mungu kwa sababu alijua yeye tu ndiye Mungu Mwenyezi. Baada ya muda, Mungu anayajibu maombi ya Ali. Haijulikani zilikuwa siku ngapi lakini inasemekana kuwa siku zilipita (ub.156). Mtunzi hajaeleza muda ambao maandalizi ya harusi ya Fatuma na Ali yalichukua, kwani inasemekana kwamba maandalizi yalifanyika. Lakini unapochunguza jinsi shughuli ya maandalizi ilivyofanyika huenda ilichukua muda mrefu ambao haueleweki. Sababu ni kuwa Mungu anamwamuru Malaika Jibrili kuwaita malaika wenzake. Jibrili anawaita na wote wanakusanyika kungojea watakayoambiwa na Mungu.

Baadaye Mungu anamwamuru Malaika Jibrili kumwambia Ridhiwani aipambe Pepo nzima, na hata wavulana na watoto wa kule Peponi wanapaswa wajipambe ipasavyo.Ridhiwani anastahili kuzipamba ghorofa nane na sehemu zote za kubarizia kwa fedha na dhahabu. Majumba yote ya Peponi yanastahili kupambwa nje na ndani na pia barabara:Malango yote ya Peponi yanastahili kufunguliwa wazi na yote ya kuzimuni kufungwa pasisalie hata mwanya wa mtu kuchungulia (ub.173-200). Kila wakati Malaika Jibrili anamwambia Ridhiwani kuwa anayomwambia yafanyike leo, 'leo'hii msomi wa utenzi huu anashindwa kama kweli yote anayoamriwa Malaika Ridhiwani yanafanyika katika siku moja au zaidi. Safari ya malaika kutoka Mbinguni kuteremsha mahari kwa Mtume Muhammad haieleweki muda iliyochukuwa. Hii ni kwa sababu inadaiwa kuwa malaika waliteremka Mbinguni kuleta mahari kwa Mtume Muhammad. Muda ambao safari hiyo inachukuwa haueleweki.

## 3.5 Wahusika na uhusika.

Wamitila (2002:18), anafafanua wahusika kama viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile na huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, anasema kuwa wahusika ni 'binadamu'

wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambuliwa na wanayoyasema (mazungumzo) na wanayoyatenda (matendo). Wamitila (2008), anafafanua dhana ya mhusika kama mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za binadamu.

Katika *Utenzi wa Mwana Fatiuma* kuna wahusika aina mbili ambao ni binadamu na viumbe ambao si binadamu. Wahusika binadamu ni pamoja na Mtume Muhammad, Ali na Fatuma nao wahusika ambao si binadamu ni Allah, Malaika Jibrili, Mikaili na malaika wengine. Wahusika ambao si binadamu ndio wanaosababisha tuuchukulie utenzi huu kama wa ajabu. Majukumu ambayo Allah na malaika wanayafanya ni ya kiajabu na ya kushangaza. Allah kwa nafasi yake anatimiza maombi ya Ali kwa ajili ya tamanio lake la kutaka kumwoa Fatuma na kumwondolea Mtume Muhammad wasiwasi aliokuwa nao kuhusu atakayemwoa Fatuma ambaye ni bintiye wa pekee. Allah anamwondolea Ali dhiki aliyokuwa nayo ya kulipa mahari kwa kuwatuma malaika wakiongozwa na Malaika Jibrili kutoka mbinguni kuyaleta duniani. Hili ni dhihirisho tosha kuwa hakuna jambo gumu mbele ya Allah kwa kuwa ana uwezo mkubwa. Allah anatimiza haja ya moyo wa Fatuma kwa kukubali tamanio lake, la kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake wa dini ya Kiislamu.

Allah ni mtetezi wa wanyonge na maskini kwani anamtetea Ali wakati hana chochote cha kumwezesha kumposa Fatuma. Baada ya harusi ya Ali na Fatuma duniani. Allah anawaondoa katika dhiki ya ufukara kwa kumtuma kijana aliyekuwa na ngamia wakati Ali alikuwa anatoka Shamu kufanya kibarua ambacho kingemwezesha kupata pesa za kuwanunulia chakula Ali na mke wake.

Allah ni mpeanaji, anapeana wakati Ali anafikiria hana mbele wala nyuma baada ya kuwasaidia maskini watatu aliokutana nao. Allah ndiye husababisha hali katika maisha ya binadamu kwani maskini ambao Ali alikutana nao kutoka Shamu, Allah ndiye alifanya iwe jinsi ilivyokuwa ndipo Ali abarikiwe zaidi. Ali anapowasaidia na peni zote alizokuwa nazo, Allah anasababisha kutokezea ghafla kwa kijana aliyekuwa na ngamia na baada ya muda kidogo kunatokezea Mwarabu anayemnunua ngamia kwa pesa nyingi. Pesa anazopata Ali zinampelekea kuwa tajiri wa kutajika.

Malaika kwa upande mwingine wametumika kama wasaidizi wa Allah. Malaika Jibrili mara kwa mara ametumika katika kuwasilisha ujumbe. Yeye ndiye anayetumwa na Mungu kuwaita malaika wengine kwa ajili ya maandalizi ya harusi ya Ali na Fatuma mbinguni. Malaika Ridhiwani ndiye anayehusika katika maandalizi na kuipamba Peponi kwa ajili ya harusi ya Ali na Fatuma. Katika ndoa kati ya Ali na Fatuma kule mbinguni Malaika Jibrili anamwakilisha Ali, Mungu anachukuwa nafasi ya hakimu wa Fatuma, Malaika Mikaili anachukua nafasi ya shehe anayewaunganisha maarusi nao malaika wengine wanne wanakuwa kama mashahidi. Malaika ndio wanaotumiwa kuwasilisha mahari kwa Mtume Muhammad kutoka mbinguni hadi duniani kwa niaba ya Ali.

Allah na malaika ni wahusika ambao si wa kawaida na kwa hivyo wanaupa *Utenzi wa Mwana Fatuma* sifa ya kiajabu. Shughuli ambazo hao wahusika wanajihusisha nazo ni shughuli za kiajabu ambazo wahusika wa kawaida hawawezi kuzifanya. Kwa mfano kuyawezesha yasiyowezekana kwa kumwezesha Ali kumwoa binti wa Mtume hata katika hali yake ya ufukara. Vilevile harusi kufanyika mbinguni baada ya malaika kuamriwa na Allah kuipamba na kuiandaa Peponi. Kusababisha harusi ya watu walio duniani kufanyika mbinguni na malaika kupeleka mahari kwa Mtume Muhammad kutoka mbinguni ni matukio ya kiajabu yanayohusisha

wahusika wa kiajabu. Kwa hivyo matukio ya kiajabu na wahusika wa kiajabu wanasababisha kuwepo kwa sifa ya kiuhalisiajabu .

### 3.6 Upanuaji wa mwanda wa kisimulizi

Wamitila, (2008) anadai kuwa riwaya za aina hii hazina mipaka wazi ya mianda ya kisimulizi (huweza kuhusisha ulimwengu dhanifu au ulimwengu wa njozi na maingiliano kati ya aina hizo tofauti kuvunjwa kiasi kwamba matukio ya ulimwengu wa njozi yanafuata kanuni zilezile za matukio ya ulimwengu halisi.

Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* sifa ya upanuaji wa mwanda wa kisimulizi. Sifa hii imedhihirika pale mtunzi wa utenzi huu ameisababisha hali ambapo hakuna mpaka kati ya dunia na mbingu, kwani matukio yanayoujenga utenzi huu yanafanyika katika sehemu hizi mbili. Tunapata maandalizi ya harusi ya Ali na Fatuma yanafanyika mbinguni (ub. 157-229). Vilevile kunakuwa na harusi kati ya Ali na Fatuma, pale wanawakilishwa na Allah pamoja na malaika (ub. 230-239). Baada ya harusi mbinguni kunakuwa na harusi duniani (ub. 240-261). Malaika wanatumwa na mahari na Allah kutoka mbinguni kumpelekea Mtume Muhammad duniani.

Kwa hivyo tunaona kuwa mpaka kati ya mbinguni na duniani umevunjwa kwa sababu matukio yanaingiliana kiasi kwamba msomi anashindwa kueleza iwapo kuna mpaka kati ya mbinguni na duniani, ufinyu umedhihirika kiasi kwamba shughuli zinafanyika kana kwamba ni vijiji viwili vinavyokaribiana. Tunapata kuwa baada ya Ali kumwomba Allah kwa ajili ya kuoa, Allah anayajibu maombi yake kwa kuwaamuru malaika kuandaa  na kuipamba Peponi. Kwa kawaida ndipo harusi ifanyike duniani huwa kuna maandalizi. Kwa hivyo baada ya Peponi kuandaliwa na kupambwa, harusi inafanyika mbinguni ambapo Allah ni hakimu wa Fatuma, Malaika Jibrili anamwasilisha Ali, Mikaili anakuwa Shehe wa kuwaunganisha maharusi nao

malaika wanne wanakuwa mashahidi. Shughuli ya harusi inafanyika Mbinguni utadhani inafanyika duniani.

Wakati Fatuma anakubali ndoa kati yake na Ali na kukataa mahari aliyoletewa kutoka mbinguni, Malaika Jibrili anapashwa habari na Mtume Muhammad. Baada ya kupashwa huo ujumbe, Malaika Jibrili anarudi mbinguni kumpasha Mungu tamanio la Fatuma. Tunaona kuwa Mungu anamtuma tena duniani ili amwambie Fatuma kuwa ombi lake limekubaliwa. Malaika Jibrili anateremka duniani huku ameibeba aya ambayo anampelekea Fatuma kama kitambulisho kuwa Mungu amekubali na kulijibu ombi lake. Kwa hakika hakuna mpaka kati ya mbingu na dunia katika matukio tuliyoyataja. Yakafanyika kana kwamba hakuna mpaka kati ya mbingu na dunia.

Kuhusu sifa za uzuri wa Fatuma tunapata kuwa sifa ya upanuaji wa mwanda wa kisimulizi imedhihirika. Hii ni kwa sababu inasemekana kuwa sifa za uzuri wa Fatuma zinaenea dunia nzima. Kila pembe ya dunia ilipata kufahamu juu ya sifa za uzuri wa Fatuma. Mtunzi anataja nchi za Uarabuni, Misri, Yaman, Uswisi, Damasika, Iraki na hata Ulaya. Hapa tunapata kuwa sifa za uzuri wa Fatuma zinaenea dunia nzima. Kwa vile sifa za uzuri wa Fatuma zinaenea dunia nzima tunapata kuwa wanaume wengi walitamani kumwoa Fatuma. Hii inapelekea wanaume wengi kupeleka posa kwa ajili ya kumwoa Fatuma. Kwa hivyo wanaume dunia nzima walimpelekea Mtume Muhammad posa kwa ajili ya kutaka kumwoa Fatuma. Inasemekana kuwa wanaume wenye vyeo vikubwavikubwa walitamani sana na kutarajia kumwoa Fatuma wakiwemo wafalme.

## 3.7 HITIMISHO

Katika sura hii, tumezishughulikia sifa za kiuhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Tumegundua kuwa huu utenzi una matukio ya kiajabu ambayo ni sifa ya kiuhalisiajabu pale ambapo harusi ya Ali na Fatuma inafanyika mbinguni. Mungu anahusika kibinafsi pamoja na malaika katika kuandaa na kutayarisha mbinguni kwa ajili ya harusi. Mungu anaandaa vyakula na kuwaalika wageni kusherehekea harusi kati ya Ali na Fatuma.

Kuvunjwa kwa mipaka ya kimaeneno ni sifa nyingine ya kiuhalisiajabu kwa sababu sifa za uzuri wa Fatuma bintiye Muhammad zimeenea kila pembe kiasi kwamba kila anayepata kuzisikia sifa za uzuri wa Fatuma anakimbia kupeleka posa kwa nia ya kutaka kumwoa . Fatuma kuposwa na wachumba ambao si wa dini ya Kiislamu ni hali ya kuvunjwa kwa mipaka ya kimaeneo kwani inasemekana kuwa hata makafiri walimposa Fatuma, wasio Waislamu waliamua kuslimu na familia zao zote huku wakitarajia kumwoa Fatuma. Sifa nyingine za kiuhalisiajabu ni pamoja na kutosonga kwa wakati pale unashangaa iwapo kwa mfano matayarisho na maandalizi ya mbinguni kwa ajili ya harusi kati ya Ali na Fatuma yalichukua siku moja au zaidi. Safari ya malaika kumpelekea Mtume Muhammad mahari kutoka mbinguni hadi duniani pia ni tukio la kiajabu. Mungu pamoja na malaika ni wahusika ambao ni wa kiajabu.

# SURA YA NNE

## UMUHIMU WA SIFA ZA KIUHALISIAJABU KATIKA UTENZI WA MWANA FATUMA.

### 4.0 UTANGULIZI

Baada ya kuzichanganua sifa za Kiusiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*, tumepata msukumo wa kutalii mchango wake katika jamii. Dini kama mojawapo ya mifumo kadhaa ya imani na ibada zake. Ndipo uweze kuwa na uamilifu wa kutekeleza, kwa kusudi la kudumisha na kusawazisha hali tofauti tofauti katika dini. Sifa za Kiuhalisiajabu huwa na fursa kubwa ya kurekebisha na kubadilisha hali ambazo si bora katika dini. Sifa za Kiuhalisiajabu hulenga kuwanufaisha waumini wa dini kwa kuhakikisha kuwa maadili yanatiliwa maanani na kufuatwa.

### 4.1.0 Umuhimu wa sifa za kiuhalisiajabu katika kuendeleza maudhui ya kidini.

### 4.1.1 Fahari ya watu wa dini

Sifa za kiuhalisiajabu ni fahari ya watu wa dini kwa sababu waumini wa dini husika hujivunia na kuuonea fahari uhalisiajabu husika. Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* kuna matukio ya kiajabu ambayo waumini wa dini ya Kiislamu huyaonea fahari na kujivunia kwa mfano sifa za uzuri wa kupindukia anazolimbikiziwa Fatuma ni fahari kwa Waislamu kwa kuwa wanaona kuwa Mwana Fatuma ni mwanamke wa kipekee ambaye kila mmoja wa dini ya Kiislamu anapaswa kujivunia. Inadaiwa kuwa ana uzuri usi na kifani, uzuri usilinganishwa na inatokezea kuwa sifa za uzuri wake zinaenea ulimwengu mzima. Inadaiwa kuwa hakuna bikira anayelinganishwa na Fatuma ambaye ni bintiye Mtume Muhammad. Sifa za uzuri wa Fatuma zinapelekea kila mmoja wa waumini wa dini ya Kiislamu kuzionea fahari na kujivunia kwani kila mwanadamu hupenda kujihusisha na sifa nzuri.

Maandalizi na matayarisho ya harusi kati ya Ali na Fatuma kule mbinguni ni jambo la kuonea fahari. Hii ni kwa sababu Mungu na Malaika wanajihusisha katika shughuli za maandalizi ya Peponi ambapo harusi hii inafanyikia. Baada ya maandalizi kunafanyika harusi mbinguni pale Mungu, malaika Jibrili, malaika Mikaili na malaika wanne wanachukua kila mmoja nafasi yake. Baadaye harusi nyingine kati ya Ali na Fatuma inafanywa duniani. Maandalizi ya harusi na kufanyika kwa harusi kule Peponi ni tukio la kifahari na la kujivunia kwa waumini wa dini ya Kiislamu kwa sababu Mungu na malaika wanahusika kikamilifu.

Mahari kuteremshwa na Mungu kutoka mbinguni kupelekwa duniani na malaika kwa Mtume Muhammad kwa niaba ya Ali kumwoa Fatuma ni tukio la kiajabu ambalo kwa waumuni na dini ya Kiislamu ni tukio la kifahari na la kujivunia kwa sababu inaonyesha kuwa Mungu ni Mwenyezi. Waumini wanajivunia tukio hili kwa sababu linawawezesha kuamini kuwa Mungu ni mtetezi wa wanyonge kwani Ali hakuwa na uwezo wa kuyalipa mahari. Lakini Mungu anamtendea muujiza kwa kumteremshia Mtume Muhammad kupitia Malaika wakiongozwa na Malaika Jibrili kwa niaba ya Ali kumwoa Fatuma bintiye Mtume Muhammad. Mahari kuteremshwa kutoka mbinguni na Mungu kwa niaba ya Ali kumwoa ni tukio la kiajabu na la kifahari kwa sababu, Fatuma anayehusishwa na dini ya Kiislamu ndiye mwanamke wa kipekee duniani aliyelipiwa mahari na Mungu kutoka mbinguni. Hapajawahi kutokea tukio kwani ni Fatuma bintiye Mtume Muhammad ndeye pekee katika dunia nzima aliyetunukiwa nafasi hii na Mwenyezi Mungu.

Fatuma anakataa mahari kutoka kwa Mungu na kuomba ombi lake halisi la kuwa mwombezi. Mungu anaikubali haja ya moyo wake na Mungu anamtuma Malaika Jibrili kumpelekea Fatuma aya ambayo anaikubali, anaifunga kwenye uzi na kujifunga shingoni. Tukio

la Fatuma kukataa mahari aliyotolewa na Mungu kutoka mbiguni ni la Kiajabu, na vile vile kule kuteremshwa kwa aya kutoka mbinguni hadi duniani kupitia kwa malaika Jibrili. Haya matukio ni fahari ya waumini wa dini ya Kiislamu kwa kuwa yanawahimiza kutokuwa na tamaa ya vitu vya ulimwengu ambavyo ni vya muda mfupi, bali wautazamie ufalme wa mbinguni ambao hauna mwisho. Fatuma anapendekezea Mungu kuwa apewe kibali cha kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake wa dini ya Kiislamu siku ya hukumu.

Baada ya harusi kati ya Ali na Fatuma duniani, wanaamka asubuhi na inatokea kuwa hakuna chakula hata kidogo. Ali anashika safari ya kuelekea Shamu kutafuta kibarua angalau apate pesa za kununua chakula. Ali alipata kibarua na analipwa peni tatu. Ali anaamua kurudi Madina na njiani anakutana na maskini watatu ambao kwa sababu ya mahitaji waliyonayo inambidi atoe peni hizo na kusalia bila. Hali anayoipitia Ali ya kutoape peni zote katika dini ya Kiislamu ni la kifahari na la kujivunia. Hii ni kwa sababu waumini wa dini ya Kiislamu wanaamini sana katika kuwasaidia watu wasi na uwezo kama maskini, vilema, wendawazimu, na wengine wengi ambao wana shida mablimbali. Waumini wa dini ya Kiislamu huonea fahari katika kusaidia kuliko kusaidiwa.

Ali anapomuuza ngamia aliyeuziwa kwa deni na kijana asiyemjua, analipwa pesa nyingi ambazo wanaandalia sherehe yao ya harusi duniani na pesa zinazosalia, Ali na Fatuma wanaamua kutoa sadaka. Ali na Fatuma wanayaonea fahari maisha ya ufukara kwani baada ya kuzipeana pesa hizo kama sadaka wanayarudia maisha yao ya ufukara ambayo kwao wanayafurahia. Kwa hivyo katika maisha ya muumini wa dini ya Kiislamu maisha ya dunia ya ahera ni muhimu zaidi kuliko ya hapa duniani.

### 4.1.2 Kitambulisho cha kidini

Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* sifa za kiuhalisiajabu ni kitambulisho cha kidini hasa dini ya Kiislamu. Kila dini ulimwenguni ina uhalisiajabu wake wa kutambulisha dini husika. Tunapata kuwa dini ya Kiislamu ina sifa ambazo zinajitokeza katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* na ambazo zinaipatia dini kitambulisho. Yeyote anayasoma matukio ya kiajabu katika utenzi huu anatambua kuwa si dini yoyote inayozungumziwa ila ni dini ya Kiislamu.

Matukio ya kiajabu yanayotambulisha dini ya Kiislamu katika *Utenzi Wa Mwana Fatuma* ni pamoja na sifa za uzuri wa mwana Fatuma ambaye ni bintiye Mtume Muhammad. Mtunzi anazielezea kwa kina sifa hizi na hata kumwacha msomaji kushangaa kwa hakika iwapo Fatuma ni binadamu wa kawaida au ni kiumbe kutoka mbinguni. Mtunzi anadai kuwa hakuna mwanamke duniani anayeweza kulinganishwa na Fatuma. Ameeleza kuwa sifa za uzuri wa Fatuma bintiye Mtume Muhammad unaenea pembe zote za ulimwengu. Mwandishi anadai kuwa sifa za uzuri wa Fatuma zilienea Uarabuni. Uarabuni ni nchi zenye imani ya Kiislamu na huko ndiko sifa za uzuri wa Fatuma zinaenea kwa kasi na kwa hivyo kudhibitisha kuwa sifa za kupindukia za uzuri wa Fatuma bintiye Mtume na kuenea kwake duniani kote kuwa kama kitambulisho cha kidini si dini yoyote ile ila dini ya Kiislamu.

Kuhusika kwa Mungu na malaika katika maandalizi na matayarisho ya harusi ya Ali na Fatuma ni tukio la kiajabu na ambalo ni kitambulisho cha kidini. Hii ni kwa sababu kuwa hakuna dini nyingine yoyote ambayo imeshuhudia hali kama hii. Tunapata kuwa Mungu anawaamuru malaika wengine wakiongozwa na Malaika Jibrili kuandaa Peponi kwa ajili ya harusi kati ya Ali na Fatuma.  Malaika wanaiandaa Peponi, wanaipamba, wanayafunga malango kuzimuni na kuyafungua wazi malango ya Peponi kwa ajili ya harusi.

Baada ya maandalizi kunakuwa na harusi Peponi pale Mungu anawakilisha Fatuma kama hakimu wake, malaika Jibrili anamwakilisha Ali, malaika Mikaili anaihalalisha ndoa na kuwaunganisha maharusi nao malaika wanne wanashuhudia shughuli ya harusi. Haya ni matukio ambayo yamefungamana na dini ya Kiislamu kwani waumini wa dini ya Kiislamu wanayosoma katika Korani Takatifu na hayapo katika vitabu vitakatifu vya dini zingine duniani. Kwa hivyo, waumini wa dini ya Kiislamu wanakubaliana na matukio haya ya kiajabu na wanayaamini kuwa ni ukweli usipingika. Kwa sababu ya kutopingika kwa matukio hayo yanakuwa kitambulisho cha dini ya Kiislamu.

Mungu kuwatuma malaika wakiongozwa na malaika Jibrili kupeleka mahari duniani kwa Mtume Muhammad kwa niaba ya Ali kwa ajili ya kumwoa Fatuma ni tukio la kiajabu na ambalo ni kitambulishi cha dini ya Kiislamu. Hata safari ya kutoka mbinguni hadi dunia iliyofanywa na malaika walipokuwa wanamletea Mtume Muhammad mahari. Haieleweki safari hiyo inachukua muda gani lakini mtunzi anadai kuwa malaika walibeba bidhaa vya thamana kulingana na uwezo wa kila mmoja. Mahari kwa kawaida hutolewa katika kijiji kimoja hadi kingine lakini katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* mahari yanateremshwa kutoka mbinguni kwa Mungu hadi duniani ambapo binadamu anaishi. Hata kuteremka kwa malaika kutoka mbinguni hadi duniani ni tukio la kiajabu kutoka mbinguni hadi duniani. Matukio haya yanatambulisha dini ya Kiislamu kwa sababu ni matukio ya kiajabu yanayoaminiwa na waumini wa dini ya Kiislamu yenye msingi katika Uislamu.

### 4.1.3 Ukombozi na muungano wa waumini

Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*, matukio ya kiajabu yanayomzunguka Fatuma bintiye Mtume Muhammad ni ukombozi na muungano wa waumini. Hii ni kwa sababu sifa za uzuri wa Fatuma hazijajikita katika jamii moja mahsusi bali dunia nzima. Inadaiwa kuwa kila pembe ya dunia ulipata kujua sifa za Fatuma bintiye Mtume Muhammad. Kujulikana kwa sifa za uzuri wa Fatuma kunachangia pakubwa katika ukombozi wa waumini ya Kiislamu kote duniani . Mtunzi anadai kuwa kwa sababu ya kuenea kwa uzuri wa sifa za Fatuma duniani kote, kia mwanamume alitamani sana kumposa na kutaka kumwoa. Waislamu, wafalme, makafiri na hata wengine waliamua kuslimu na familia zao kwa kusudi la kutaka kumwoa Fatuma.

Fatuma anakataa mahari iliyotolewa na Mungu kwa niaba ya Ali na Kumwomba Mungu ampatie kibali cha kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake wote wa dini ya Kiislamu. Hapa tunagundua kuwa Fatuma anataka kuwa katika hali ya kuwakomboa na kuwaunganisha wanawake wote wa Kiislamu kote ulimwenguni. Fatuma hataki kuwatetea tu wanawake waislamu walio Madina pekee yake bali anataka awaombee na kuwatetea wanawake wote wa dini ya Kiislamu kote ulimwenguni. Anamsihi mume wake asimtoe hirizi shingoni atakapokufa kwani hiyo ndiyo itamtambulisha mbele ya Mungu Kuwa yeye ndiye mwombezi na mtetezi wa wanawake ulimwenguni na kuwa Mungu ndiye atamtoa hiyo hirizi shingoni.

Ali kuelekea Shamu alikoenda kufanya kibarua ya kupata pesa za kununulia chakula inaashiria ukombozi na muungano wa waumini. Hii ni kwa sababu baada ya Ali kufanya Kibarua, analipwa peni tatu ambazo akiwa njiani anakutana na maskini watatu ambao anawasaidia. Ali hakuwasaidia kwa sababu anawajua lakini ilibidi awakomboe katika hali ambayo walikuwa nayo ya umaskini. Ali anawasaidia si kwamba ni watu anawaelewa lakini

kwa ajili ya kuwakomboa na kuhakikisha muungano kati ya waumini unadumishwa, anaamua kuwasaidia na kusalia bila chochote.

### 4.1.4 Ukuzaji wa imani ya kidini

Matukio ya kiajabu katika *Utenzi wa Mwana wa Fatuma* yametumiwa ili kukuza imani ya dini ya Kiislamu. Maandalizi na matayarisho ya Peponi kwa ajili ya harusi kati ya Ali na Fatuma ni tukio la kiajabu ambalo kila muumini wa dini ya Kiislamu. Unapofika wa ndoa, waumini wengi wa dini ya Kiislamu huamini ndoa ni takatifu na hakuna aliye na uwezo isipokuwa Allah ambaye ni Mungu Mwenyenzi. Waislamu wana imani kuwa ndoa hufanyika kwanza mbinguni na baadaye duniani ambapo Mungu mwenyewe na malaika hujihusisha kikamilifu, kila mmoja akitekeleza wajibu wake.

Kuwepo kwa viumbe mbinguni ambao si wanaume na si wanawake ni tukio la kiajabu ambal linasaidia kukuza imani ya kidini. Hii ni kwa sababu watu wanaaamini kuwa hali hii inapelekea kuwa swala la ndoa mbinguni halipo. Kwa hivyo shida na matatizo ya ndoa watayaaacha duniani na kuwa mbinguni ni raha mstarehe. Kwa hivyo kutokuwepo kwa waume kwa wake mbinguni kunapelekea waumini kuamini kuwa maisha ya mbinguni ni bora zaidi kuliko duniani.

Wakati Ali hana chochote cha kulipia mahari, Mungu anawaamuru malaika mbinguni kuteremka duniani wakiwa wamebeba mahari kila mmoja kiasi anachoweza kumpelekea Mtume Muhammad kwa ajili ya Fatuma. Hapo tunauona uwezo mkubwa alionao Mungu na kuwa linaloonekana kwa binadamu gumu kwake Mungu ni rahisi sana. Hili tukio la kiajabu limetumika ili kukuza imani ya muumini wa dini ya Kiislamu. Anayekumbana na tukio hili anaamini kuwa kwake Mungu yote yanawezekana hata yale binadamu anafikiria hayawezekani

Mungu Mwenyezi ana uwezo. Pale muumini ana fikira kuwa hana mbele wala nyuma anapata tumaini kuwa Mungu anayewajali walio wanyonge, na kuwa yeye ndiye mtetezi wao jinsi alivyomtetea Ali kwa kumlipia mahari na kumpa kibali cha kumwoa Fatuma.

Katika safari ya Ali kuenda Shamu kutafuta kazi, baada ya kulipwa peni tatu, anarudi Madina, njiani anakutana na maskini na maskini watatu ambao wanamwomba pesa. Ali anawapatia peni zote tatu na kusalia bila. Ali akiwa anafikiri atakachokifanya kwa vile amepeana pesa zote alizolipwa na nyumbani hakukuwa na chochote cha kula na mke wake. Kunatokea kijana aliyekuwa na ngamia, hawajuani lakini kijana anamuuzia ngamia kwa deni. Ghafla panatokezea mwarabu anayemnunua ngamia kwa kiasi kikubwa cha pesa. Ali anakuwa tajiri bila kutarajia. Matukio haya yanakuza imani ya kidini kwa sababu hali hizi zimesababishwa na Mungu. Mungu anamjaribu Ali kupitia kwa hao maskini ili aone iwapo Ali alikuwa mwaminifu.

Kupitia kwa kijana aliyekuwa na ngamia na Mwarabu aliyemnunua ngamia, uaminifu wa Ali unalipwa na Mungu kupitia kwa kijana aliyekuwa na ngamia na mwarabu aliyemnunua ngamia kwa pesa nyingi. Matukio haya yanamsaidia muumini wa dini ya Kiislamu kukuza imani yake. Kwa hivyo muumini anastahili kujua kuwa hata jambo lolote gumu likitokezea, anakumbana nalo akiwa na matarajio kuwa Mungu ana kusudi na kuwa ataitatua hali hiyo. Matukio haya ya kiajabu yanamtia muumini matumaini katika kila hali na kwa hivyo imani inaendelea kukua hata kama hali inaonekana haistahimiliki.

Mungu kumtimizia Fatuma bintiye Mtume Muhammad haja yake kwa kumteremshia aya, kutoka mbinguni kupitia kwa malaika Jibrili ni tukio la kiajabu. Kwa muumini wa dini ya Kiislamu ni tukio la kukuza imani kwa sababu kila muumini anakuwa na imani kuwa jinsi Mungu alimtimizia Fatuma haja ya moyo wake ndivyo atakavyomtimizia. Hali hii inachangia

pakubwa katika kukuza imani ya waumini kwa kuwa wataendelea kuomba bila kukoma wakitarajia maombi yao kujibiwa jinsi Mungu alijibu ombi la Fatuma.

Ali na Fatuma wanaamua kupeana pesa walizosalia nazo kama sadaka ya Ali kumuuza ngamia pesa nyingi na kuandaa sherehe ya harusi yao duniani. Wanasalia kuwa maskini jinsi walivyokuwa mwanzoni. Kulingana na Ali na Fatuma wanaonelea kuwa mali ya hapa duniani hayana maana mali ya mbinguni. Ali na Fatuma wanaamua kupeana sadaka msikitini ili ifanye kazi ya Mungu. Kwa hivyo Ali na Fatuma wanawakilisha mfano mzuri kwa waumini wengine ambao wanastahili kuipatia kazi ya Mungu kipau mbele kuliko kuyajali maslahi yao wenyewe. Kwa hivyo kwa kutumia mali yako katika kazi ya Mungu, hali hii inachangia pakubwa kukua kwa imani ya muumini katika dini husika.

### 4.1.5 Ruwaza ya kufuatwa kama dini.

Ruwaza ni mfano wa hali au jambo. Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma,* uhalisiajabu huchangia pakubwa katika kuimarisha ruwaza bora ya kufuatwa na waumini wa dini hasa ya Uislamu. Katika utenzi huu mtunzi amezieleza sifa za uzuri wa mwana Fatuma bintiye Mtume Muhammad na jinsi zimeenea katika pembe zote za dunia. Kwa hivyo uhalisiajabu wa kuzitajia sifa kupindukia zinazoenea dunia nzima na kupelekea kila mwanamume kumposa Fatuma kwa nia ya kutaka kumwoa huchangia pakubwa ruwaza bora ya kufuatwa na Waislamu. Fatuma anakuwa mfano bora zaidi ambao unastahili kuigwa na mtoto wa kike yeyote yule wa dini ya Kiislamu ili kuendeleza sifa za mtangulizi wao mke bora zaidi kati ya wanawake wote. Kila mzazi anatumaini kuwa mtoto wake wa kike afuate nyayo za Fatuma ambaye ni mwanamke wa kuigwa.

Harusi kati ya Ali na Fatuma inafanyika mbinguni baada ya Mungu kuwaamurisha malaika wakiongozwa na Malaika Jibrili kutayarisha Peponi. Mungu na malaika wanachukua kila mmoja nafasi yake katika harusi hiyo. Hali hii inachangia katika kuwepo kwa ruwaza bora ya kufuatwa na waumini wa dini ya Uislamu. Hii ni kwa sababu waumini wa dini wanafuata ruwaza iliyotangulizwa na Mungu mwenyezi wakati wa harusi kati ya Ali na Fatuma. Waumini wa dini ya Kiislamu wanatilia maanani sana swala la ndoa na wao hulichukulia kwa uzito mwingi. Waumini wa dini ya Kiislamu wana imani kuwa maharusi huunganishwa mbinguni, na duniani ni kuweka mhuri kwa yale tayari yamekubalika mbinguni.

Swala la ndoa hasa kufanyika kwa harusi, hutiliwa maanani kwa kuwa waumini wa dini ya Kiislamu hufuata mfano kama ulivyokuwa mbinguni kwa kuandaa na kutayarisha mahali patakapofanyika harusi. Baada ya maandalizi harusi hufanywa ndani ya msikiti na wageni wanaalikwa, kunakuwa na kusherehekea jinsi ilivyokuwa mbinguni pale inadaiwa Mungu mwenyewe alikiandaa chakula na kuwaalika wageni ili washerehekee.

Uhalisiajabu unachangia pakubwa katika ruwaza bora kufuatwa na wanadini kwa sababu ufukara aliokuwa nao Ali haungemwezesha kulipa mahari kwa ajili ya kumuwoa Fatuma lakini Mungu anawatuma malaika wakiongozwa na Malaika Jibrili kumpelekea mahari yenye dhamana kwa mfalme Muhammad kwa niaba ya Ali kwa ajili ya kumwoa Fatuma.

Kwa hivyo mahari anateremshwa kutoka mbinguni hadi duniani kuonyesha ukuu wa Mungu na kuwa yeye ni Mungu mwenyezi. Uhalisiajabu huu unawafanya waumini wa dini ya Kiislamu kujua kuwa hawatakikani kuchukulia watu jinsi walivyo au kuwadharau watu kwa sababu ya hali zao za kimaisha. Unawasaidia kuelewa kuwa Mungu ndiye mwenye mali na kuwa ana uwezo katika kila jambo.

Fatuma anakataa mahari aliyoletewa kutoka kwa Mungu ambaye amewatuma malaika kutoka mbinguni. Fatuma anapeana haja ya moyo wake ya kutaka kuwa mkombozi na mwombezi wa wanawake wa dini ya Kiislamu. Mungu anakubali haja ya moyo wake na kumtuma malaika Jibrili na aya kutoka mbinguni ambayo anaifunga kwenye uzi na kujifunga shingoni mwake. Fatuma anamsihi mumewe kuwa hata atakapokufa aya hiyo isindolewe shingoni mwake, kwa kuwa kitakuwa kitambulisho wakati atakuwa mbele ya Mungu. Fatuma kukataa mahari na kutamani kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake wa dini ya Kiislamu ni mfano mwema wa kufuatwa na waumini wa dini ya Kiislamu. Hii ndiyo sababu waumini wa dini ya Kiislamu mara kwa mara wanaombeana wenyewe kwa wenyewe, wanawaombea maswahibu, viongozi wao wa dini, na kiongozi wao Mtume Muhammad.

Baada ya harusi kati ya Ali na Fatuma, siku inayofuata hawana chakula, Ali anaamua kuenda Shamu kutafuta kibarua ili apate pesa za kununulia chakula. Ali anapata kazi ambayo baada ya kuifanya analipwa peni tatu. Njiani anakutana na maskini watatu ambao wanamwomba usaidizi, anawahurumia na kuwasaidia pesa zote na kusalia bila chochote na huku hana chakula nyumbani jambo hili halikuwa la kawaida. Uhalisiajabu huu ni ruwaza bora ya kufuatwa na waumini kwa sababu inawawezesha kujua kuwa kila mmoja anastahili kumbebea mwenzake mzigo. Waumini wanajiweka katika nafasi za wenzao walio katika shida fulani na kwa kufanya hivyo Mungu mwenyezi anawabariki. Mfano wa Ali na Fatuma umeigwa kwani waumini wa dini ya Kiislamu wakati wa Ramadhani huwasaidia maskini mali zao na kuwasaidia wenye shida mbalimbali.

Waumini wa dini ya Kiislamu hutilia mkazo kutoa zaka na sadaka katika misikiti. Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*, Ali anauziwa ngamia kwa deni na kijana asiyemjua na baadaye anamuuzia Mwarabu ambaye anampatia pesa nyingi. Ali anakuwa tajiri na kwa hivyo yeye na

mke wake wanaandaa sherehe kubwa ya harusi na kuwaalika wageni na kusherehekea, pesa zilizosalia Ali na Fatuma walizitoa zote kama sadaka na kurudia hali yao ya umaskini. Huu ni mfano ambao umeigwa na waumini wa dini ya Kiislamu kwa kuwa wao hulipa zaka na sadaka misikitini, pesa ambazo hutumika kwa ajili ya kazi ya Mungu mwenyezi.

### 4.1.6 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia umuhimu wa uhalisiajabu katika kuyaendeleza maudhui ya kidini. Tumegundua kuwa uhalisiajabu huchangia pakubwa katika kuendeleza maudhui ya kidini kwa sababu uhalisiajabu huwa; fahari ya watu wa dini, kitambulisho cha kidini, ukombozi na muungano wa waumini, ukuzaji wa imani ya kidini na ruwaza ya kufuatwa kama dini

## SURA YA TANO

### 5.0 MAHITIMISHO.

Katika sura hii, tumetoa mahitimisho ya utafiti wetu ambao ulishughulikia sifa za kiuhalisiajabu na umuhimu wake katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.* Nadhari tuliyoitumia katika utafiti huu ni ya uhalisiajabu. Nadhari hii ilifaa sana katika uhakiki wetu kwa kuwa imethibitisha kuwa uhalisiajabu ni muhimu katika kuendeleza maudhui ya kidini katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.* Matukio ya kiajabu, sifa za kiuhalisiajabu huchangia katika kuyaendeleza maudhui ya kidini.

Katika sura ya kwanza, tumeshughulikia maswala ya kimsingi yanayojenga utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, nadharia tete, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na njia za utafiti tulizotumia.

Nadharia tete yetu ya kwanza katika utafiti huu ilikuwa matukio ya kiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.* Ya pili ilikuwa, sifa za kiuhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.* Nadharia tete ya tatu na ya mwisho ilikuwa, uhalisiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* una umuhimu katika kuendeleza maswala ya kidini. Katika sura ya pili, ya tatu na ya nne, tumezitathimini kwa undani nadharia tete hizi katika kuchanganua mada yetu.

Katika sura ya pili tuliuhakiki kimhtasari *Utenzi wa Mwana Fatuma* .Tulishughulikia maisha ya Fatuma bintiye Mtume Muhammad tangu utotoni hadi anapofikia umri wake wa kuolewa. Tuliziangazia sifa za uzuri wake Fatuma ambazo amelimbikiziwa kupita kiasi. Tulipata kuwa sifa za uzuri wa Fatuma zilienea duniani kote na kupelekea kila aliyesikia kutamani kumposa na kumwoa. Mungu anamwandalia Fatuma harusi mbinguni kupitia kwa malaika. Harusi inafungwa mbinguni kati ya Ali na Fatuma ambaye hakuwa na mali yoyote. Mungu anateremsha mahari kutoka mbinguni hadi duniani kupelekwa kwa Mtume Muhammad kwa

niaba ya Ali. Harusi inafanyika duniani kati ya Ali na Fatuma ambao wanabarikiwa na watoto wa kiume wawili ambao ni Hasani na Huseini.

Vilevile tulichanganua matukio ya kiajabu yanayoibuka katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Baadhi ya matukio haya ni pamoja na; uzuri wa kupita kiasi alionao Fatuma unaopelekea sifa kuenea pembe zote za dunia. Hali inayopelekea wanaume kila pembe ya dunia kupeleka posa kwa kutaka kumwoa Fatuma. Mungu anaiandaa harusi kati ya Ali na Fatuma mbinguni kwa kuwahusisha malaika. Mungu anawaamuru malaika kupeleka mahari kutoka mbinguni hadi duniani kwa niaba ya Ali ambaye ni maskini kwa ajili ya kumwoa Fatuma bintiye Mtume Muhammad. Fatuma anateremshiwa aya kutoka mbinguni kupitia kwa malaika Jibrili baada ya Fatuma kukataa mahari ya thamana. Haja ya Fatuma ni kuwa mwombezi na mtetezi wa wanawake wa dini ya Kiislamu. Baada ya Ali kufanya kazi Shamu anawasaidia maskini pesa zote alizolipwa, ghafla panatokea kijana aliyekuwa na ngamia na kumuuzia kwa deni. Ali na kijana huyo hawafahamiani lakini shughuli ya kukopeshana inafaulu. Punde panatokezea Mwarabu anayemnunua ngamia kwa pesa nyingi sana.

Kwa ajili ya kuibuka kwa matukio ya kiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*, nadharia yetu ya uhalisiajabu ilijitokeza kuwa ya muhimu na ya kufaa katika kuishughulikia mada yetu. Katika sura ya tatu ndipo sasa tulishughulikia sifa za kiuhalisiajabu, zinazoibuka katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Tulionelea kuwa ilikuwa ni lazima kuupa kipao mbele uchambuzi wa matukio hayo ya kiajabu ndipo matukio hayo ya kiajabu yabaini sifa za kiuhalisiajabu. Sifa za kiuhalisiajabu tulizoshughulikia zilikuwa; matukio ya kiajabu ambayo ni ya kushangaza na ya kuogofya. Baadhi ya matukio yanayoshangaza na kuogofya ni pale mtunzi anadai kuwa uso wa Fatuma una nuru iliyo na mwanga mkuu kuliko wa mwezi na kuwa yeyote anayemwona anatosheka kabisa. Inashangaza kuwa sifa za uzuri wake zinaenea duniani kote hivyo

kuwapelekea wanaume kutoka pembe zote za dunia kutuma posa kwa matumaini ya kumwoa Fatuma. Harusi kati ya Fatuma na Ali kufanyika mbinguni na Mungu na malaika kuhusika kikamilifu.

Sifa nyingine ni kuvunjwa kwa mipaka ya mahali ambapo shughuli za harusi kati ya Ali na Fatuma zinafanyika mbinguni na duniani. Mtunzi anadai kuwa sifa za uzuri wa Fatuma zilienea duniani nzima na hata waliomposa walitoka pembe zote za dunia.

Tuliona kuwa matukio yanayozungumziwa na mtunzi ni ya kifantasia kwa kuwa anayetunga utenzi huu hakuyashuhudia matukio anayoyatungia. Inawezekana iwe mtunzi alifikiria aliyoyatunga katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Sifa nyingine ya kiuhalisiajabu ni kuwa wakati hausongi kwa sababu haieleweka muda ambao maandalizi na matayarisho ya harusi kati ya Ali na Fatuma yalichukua. Hata mahari kuteremshwa kutoka mbinguni hadi duniani kuna wahusika ambao ni wa kiajabu kama vile Mungu na malaika wahusika wengine si wa kiume na si wa kike.

Katika sura ya nne, tulishughulikia umuhimu wa uhalisiajabu katika kuyaendeleza maswala ya kidini. Tulionyesha umuhimu wa uhalisiajabu ambapo huwa fahari ya watu wa dini, huchangia pakubwa katika kukomboa na kuwaunganisha waumini, huleta mabadiliko katika dini. Tulipata kuwa uhalisiajabu hukuza imani ya kidini, huwa kioo cha kidini, kitambulisho cha kidini na ruwaza bora ya kufuatwa utafiti huu umechunguza matukio ya kiajabu.

## 5.1 Mapendekezo

Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Tumezichanganua sifa za kiuhalisiajabu na muhimu wa uhalisiajabu. Tumeonyesha jinsi matukio ya kiajabu yanachangia katika sifa za kiuhalisiajabu. Hata hivyo tumejikita katika umuhimu wa uhalisiajabu kuyaendeleza maudhui

mahsusi ambayo ni ya kidini. Tunapendekeza kuwa watafiti wengine washughulikie mada hii kwa kuuchunguza umuhimu wa uhalisiajabu katika kuyaendeleza maudhui mengine katika utenzi huu.

**Marejeleo**


Chanady, Amaryll Beatrice. *Magical Realism and the Fantastic*. New York: Garland Publishing, Inc, 1985.

Cooper, Brenda. *Magical Realism in West African Literature*. London: Routledge Publishing, 1998.

Danow, David K. *The Spirit of Carnival: Magical Realism and the Grotesque*. Kentucky: The University Press of Kentucky,1995.

Hussein, E, N (1969). *Kinjeketile.*Oxford University Press

Kimani N. na Rocha C; (2008): *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu,* Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Maganju, J; (2004): ‘’Uhakiki wa Uhalisiajabu katika Bina-Adamu (2002) na Babu Alipofufuka (2004)’’ . Tasnifu ya M.Aya Chuo Kikuu cha Kenyatta(Haijachapishwa).

Mayor, A. W (1955): *Thuond Luo.* Nairobi: Kenya Highway press.

Mbatia, M; (2002): *Kamusi ya Fasihi :*Nairobi. Standard Textbooks.

Mbunda, M (1993): *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. East African Educational Publishers Limited.

Morrison, T (2004): *Beloved*.Vintage

Nyambuga, V.A, (2005): ‘‘Uhakiki wa Bina-Adamu! (2002) na Musa Leo (2004) na Wamitila K. W’’ Tasnifu ya M.Aya Chuo Kikuu cha Nairobi(Haijachapishwa).

Onyango-Ogutu,B.na A.A Roscoe (1974): *Keep my words*: Nairobi:East African Publishing house.

Olali, T (2010). Structure and Anti-Structure of a Swahili New Novel: Astylistic Analysis of *Babu Alipofufuka.*

Okri, B (1991): *The Famished Road. London*:Vintage.

Rogers, B. H (2002): *Word Work: Surviving and Thriving as a Writer*, Invisible Cities Press

Rio, F; (2002): *Margical Realism Definitions.* Found on internet (Unpublished).

Shaban, R (1991):*Kusadikika*.Mkuki na Nyota Publishers.

Silko, L.M (1977): *Ceremony*.Penguin.

Strecher, M. C (1999). Magical Realism and the Search for Identity in the Fiction of Murakami Haruki, Journal of Japanese Studies, Volume 25.

Wafula, R. M na Njogu; (2007): *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula R.M (1999): *Uhakiki wa Tamuthilia,Historia na Maendeleo yake*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W; (2002): *Uhakiki wa Fasihi Misingi na vipengele vyake.* Nairobi. Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K.W; (2003): *Kichocheo cha Fasihi*.Nairobi. Focus Publication ltd.

Wamitila, K. W; (2008): *Kanzi ya Fasihi-Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi,* .Nairobi. Vide Muwa Publishers Limited.

Wamitila, K.W; (2009): *Bina-Adamu*.Nairobi.Phoenix Publishers,

Wa Mutiso ,K; (2002): '*The Epic of Prncess Fatuma'*(Mswada).

Zamora, P. L na Faris, B.W (1995): *Margical Realism Theory: History Community,* London. Duke University Press.